

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS ,

GITHUNGURI CONSTITUENCY, HELD AT

P.C.E.A KIGUMO CHURCH

ON

24TH , APRIL 2002

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, GITHUNGURI CONSTITUENCY HELD AT P.C.E.A. KIGUMO CHURCH, 24TH APRIL, 2002.

Present

Com. Prof. A. I. Salim
Com. Kavesta Adagala
Com. Dr. Mosonik Arap Korir

Secretariat In Attendance:

George Naholi – Programme Officer
Charity – Assistant Programme Officer
Hellen Kanyora – Verbatim Reporter

The meeting started at 10.00 a.m with Com. Salim in chair.

Com. Salim:(inaudible) mumeamka salama, twashukuru. Muriega?

Response: Turiega muno.

Com. Salim: Tunaanza kujifunza kidogo kidogo neno hapa na pale na ndiyo njia nzuri ya kuwasiliana. Tunafurahi sana kuwa tuko na nyinyi hivi leo, na wenzangu wawili Commissioners, upande wangu wa kushoto yuko Commissioner Kavesta Adagala -- haswa kulia. Na upande wangu wa kushoto ni Dr. Mosonik Arap Korir ambaye pia ni Commissioner. Kwa hivyo leo mna team kubwa ya kusikia maoni yenu, na pia tunao staff members wetu kwa upande wa kushoto pia yuko Programme Officer wetu George Naholi, na pamoja na yeye, ni wasichana wawili kutoka kwa ofisi yetu kuu; yuko Charity wa kati kati pale ambaye anacheka na sasa anawasalimia, na yuko pia mwenzake hapo Hellen ambaye wamekuwa wote watatu hao wamekuwa wakitembea na sisi katika kila eneo, hili (hii kazi kubwa hiyo) kuhakikisha kwamba kila neno linalosemwa hapa, linarekodiwa maana si sisi tu kuandika lakini na lakini ili kuhakikisha kwamba hakuna makosa hakuna jambo ambalo litawachwa, wao pia wanarekodi. Wanaandika na pia machine yao inanasa kila neno. Tatu, yuko hapa District Coordinator wetu, Bwana Kariuki na wako pia committee members, Bwana Chairman Kiama Gitau, Chairman of committee na Reverend, bila shaka nyote mwamjua, na nitamshukuru mbele yenu nyote kwa kutupa nafasi ya kutumia kanisa hili takatifu kwa kazi hii muhimu ya kiinchi. Na nafikiri wanachama wengine wa kamati watafika baadaye kuungana nasi

Kabla kuendelea na kazi yetu ya kukusanya maoni yenu, ningependa Reverend atusomee dua, maombi kabla kuendelea mbele.

Reverend: Ningependa hasa kwanza kuwasalimu nyote, na pia kuwakaribisha katika kanisa hili, kuwashukuru, hasa Commissioners na wale -----(inaudible) na sehemu hii ya Kiambu kwa kuchagua kuja sehemu hii yetu, na hasa kuchagua kukutana katika kikao hiki. Tunashukuru sana kwa sababu ya kufanya hivyo. Nimesema nimewakaribisha, mjisikie muko nyumbani, mjisikie muko mahali ambapo ni patakatifu na yatakayotoka sehemu hii nadhani yatakuwa ya muhimu sana katika nchi yetu ya Kenya. Na kwa sababu mambo yote mazuri yatokana naye Mungu ni heri kabla ya kuanzisha jambo lolote, kwanza tuombe ili tujiweke mbele zake Mungu, atuongoze hasa hata kwa kutoa maoni yetu. Na tuombeni.

Mtakatifu Mungu wetu wa mbinguni, tumekuja mbele zako asubuhi hii ya leo, ili tukutolee shukrani zetu nyingi kwa vile umekuwa pamoja nasi tangu asubuhi tulipoamka na ukaanza pamoja nasi katika shughuli zetu za mchana wa leo. Tunasema asante kwa sababu ya kutufikisha saa hii na kutuleta katika kikao hiki. Hasa tunashukuru kwa ajili ya Commissioners wetu ambao Mungu umewaongoza na kuwafikisha katika mahali hapa. Ni safari ndefu ambayo wamefunga, na ni upendo mwingi ambao tumeona. Tunaona kujitolea kwao ndiposa tunashukuru jina lako takatifu. Tunataka kutoa shukrani nyingi kwako kwa wananchi wa sehemu hii yetu ya Karatina ambao umewafungua hili waweze kufika katika kikao hiki kutoa maoni yao: vile wangependa nchi hii yetu iendelee na iongozwe na idumishwe, Mungu wetu wa mbinguni. Ndiposa tunataka wakati huu kujiweka mikononi mwako ili Baba wetu uchukue roho zetu, fikira zetu na utuongoze. Ndiposa yale yote ambayo tutakayotoa, yawe ni maoni yenye manufaa si ya kwetu sisi tu, bali kwa nchi yetu ya Kenya. Tuongoze, kaa pamoja nasi na utubariki kwa kuwa tumeomba na kuamini katika jina la Yesu Kristo mwokozi wetu. Amen.

Mungu awabariki sana, mkiendelea kutoa na kukusanya maoni. Bwana awabariki sana. Thank you, feel at home.

Prof. Salim: Asante sana Rev. kwa kutukaribisha zaidi kwa ombi lako, ambalo lilikuwa ni ombi linalojaza moyo na akili pia. Sina haja ya kueleza umuhimu wa kazi hii kwa maana Rev. ameeleza vizuri sana kwamba hii ni kazi ambayo inahusu si sisi tu tunaoishi hivi leo katika nchi yetu lakini inahusu pia vizazi vijavyo. Ikiwa Katiba mpya itakuwa nzuri, itasaidia nchi yetu, itasaidia watoto wetu na wajukuu wetu. Kwa hivyo sisi tukiwa Commissioners tunahisi uzito wa kazi yetu lakini kama ambavyo wamesema wenzangu katika mikutano mingine, uzito na kazi kubwa ya wananchi ni kubwa kuliko yetu. Maana ni maoni yenu nyinyi ambayo mwishowe yatategemewa katika kuandika Katiba. Sisi tunasikiza, baadaye tutakwenda kusikiza maoni yenu katika kanda, kisha yataandikwa. Tutaandika Katiba kufuatia maoni ya wananchi, si maoni yetu sisi. Kwa hivyo shughuli yenu na wajibu wenu nyinyi ni kubwa kuliko yetu. Sisi yetu ni kubwa, lakini yenu ni kubwa zaidi. Kwa hivyo bila shaka mambo hayo mumelezwa na District Coordinators na wale jamaa ambao wanahusika na civic education, ambao wawili au watatu kati yao wako na sisi hivi leo. Huu si wakati wa kueleza mambo hayo yameshaelezwa, kwa hivyo ningependa kuenda moja kwa moja katika kazi ya kuwasikiza nyinyi mkitoa maoni yenu na kuyatia katika record zetu na pia vitabu vyetu. Lakini kabla kusema hivyo au kuanza kazi hiyo, ningependa kuwaeleza kwa ufupi kabisa jinsi ambavyo tutakusanya maoni yenu.

Kuna njia mbili ambazo yeyote kati yenu anaweza kutumia kutoa maoni yake. Mtu anaweza kutoa maoni yake kimdomo tu, kikauli. Atakuja hapa atatoa maoni yake na tutachukua maoni yake.

Njia ya pili, ni kwa njia ya mswada au memorandum yaani maoni ambayo mumekwisha kutayarisha na mumekuja hapa hili kutupa. Njia hizo mbili. Sasa ikiwa ni maoni ya mdomo, tutampa kila mwananchi dakika kumi kutueleza maoni yake. Ikiwa ameandika mswada au memorandum tutampa dakika tano tu. Sababu ni nini? Sababu ni kwamba yote yako katika karatasi, tutachukua, tutasoma na kupeleleza. Kwa hivyo hana haja kuisoma. Atakalofanya katika dakika tano hizo ni kutueleza kwa ufupi kabisa yaliyomo, mimi katika mswada huu, memorandum hii, nimeshtakia jambo hili na hili na lile. Naamini ni muhimu zaidi hii. Pamoja na mashtaka yangu ningependa haya yafanywe ili kustawisha mambo. Jambo hili listawishwe kwa njia hii. Jambo hili badala ya jambo hili, tufanye hili. Yaani haitoshi kushtaki lazima uwe na constructive ideas; maoni ambayo yatatufaa sisi, yatatusaidia katika kujua pendekezo na pendeleo lenu.

Tatu, ni kukumbuka jambo moja kwamba wakati tulionao hivi leo ni mfupi. Lazima tumalize saa kumi na mbili na kutakuwa na break ya lunch ndogo, kwa hivyo kila mwananchi amfikirie mwenzake. Atoe maoni yake wazi wazi, focused opinions, katika dakika zile kumi. Asitupe historia ya mashtaka hayo. “Barabara hii imekuwa imevunjika zaidi ya miaka kumi, hakuna linalofanywa na sisi tunalipa kodi”. Haya ni malalamiko hakika nzuri. Lakini asichukue wakati kueleza, sisi ni wananchi pia, ni wakenya. Tunajua hali ya Kenya, ya kijamii, ya kiuchumi na ya kisiasa. So assume that we know the problems. Muhimu zaidi ni nyinyi kutueleza ni jinsi gani tunaweza kubadilisha mambo. Kama vile maoni ya jinsi ya kubadilisha hali yetu ya kisiasa, kiuchumi, ya kitamadumi pia. Hivyo tafadhalini mkija hapa mbele mfikirie sana wakati Mtu akipewa dakika kumi, asichukue kumi na tano. Akipewa tano asichukue nane ili mwenzake aweze kupata nafasi kueleza maoni yake. Tungependa kama tulivyofanya jana, kuondoka hapa baada ya kila mmoja wenu ambaye amejandikisha hapa, kuweza kutoa maoni yake na anarudi nyumbani bila kuwa na uchungu kwamba: “Mimi nilikwenda nikakaa mpaka saa kumi na mbili mpaka hawa jamaa

wakaondoka. Hawakunipa nafasi ya kutoa maoni”. This is a peoples’ giving Constitution, we want the people to speak and give their views. Nafikiri tumefahamiana hapo. Na baada ya hayo nafikiri tunaweza kuendelea sasa, tuna jamaa waliokwisha kujiandikisha,--

Interjection: -----(inaudible)

Prof. Salim: Na muwe huru kutoa maoni yenu bila hofu yeyote by the way. Hatunasi maoni ya watu ili kwenda kuwashtaki. This is an independent Constitution; ni independent Commission. Kwa hivyo sisi tuna haki ya kusikiza maoni yenu na hakuna ambaye ana haki ya kuwasimamisha nyinyi au kuwanyamanzisha au kuwaadhabisha au kuwashtaki. Kwa hivyo be free to speak your views fearlessly and in full confidence that you are safe to do so, very important. Languages will be English and Kiswahili, largely. Lakini ikiwa yuko mwananchi ambaye anapata taabu kusema kiingereza na vile vile Kiswahili, aweze kusema lugha yake ya kikabila tuseme in this area, Kikuyu. Lakini tukumbuke kwamba akisema Kikuyu itabidi kutafsiri na hiyo inachukua wakati. Kwa hivyo tunaomba ikiwa unaweza kusema Kiswahili, tafadhali utasema Kiswahili. Ikiwa huwezi Kiswahili na kiingereza, una ruhusa ya kusema Kikuyu na tutajaribu kutafsiri. Sasa moja kwa moja kwa yule wa kwanza kabisa aliyejiandikisha hapa, yeye ni Bwana Kuria Kagori na anatoa maoni ya kimdomo. Bwana Kuria. Karibu. Tafadhali utaangalia wakati. Tunakupa dakika kumi lakini ukimaliza dakika tano pia, itakuwa vizuri.

Bw. Kuria Kungu Kagori: Haya asante sana, yangu ni kuangalia kidogo tu. Nataka kuongea mambo ya Education Act. Kwanza nataka kuguzia kitu kinaitwa PTA. Jina yangu ni Kuria Kungu Kagori na mimi ni mwenyeji wa hapa Komothai Location. Katika hiyo nimetaja yaani Education Act, juzi tulikuwa na mambo ya cost-sharing. Mzazi siku hizi ndiyo anahusika na kugharamia mambo ya masomo. Makosa makubwa sana katika Katiba ya leo ni kwamba PTA haishughuliki na Act ya masomo, Education Act. Tukiaangalia, tunaambiwa kwenye ministry kuwa Education Act inatambua Board of Governors, na pengine kuna Board of Governors na Board of Trustees. Maoni yangu ni kwamba masomo siku hizi yako kati ya mzazi na Serikali: agharamie mijengo na karo na mambo mengine, nayo Serikali ilipe mwalimu. Kwa hivyo naona ya kwamba Board of Governors iondolewe pamoja na Board of Trustees. Tuunde PTA ambayo ni muungano wa wazazi na waalimu na ihakikishwe kikatiba. Pia PTA iangalie mambo ya masomo yote, kuanzia nursery school mpaka university.

Haya, tukija upande wa kilimo, mkulima wa Kenya hana haki ya kuuza mazao yake. Kunazo Boards kama ya kahawa, ya majani ya chai, na maziwa. Hizi boards zinaongozwa na watu wanaochaguliwa na Serikali na wakati mwingi si wakulima. Sisi tumekuwa na mswada wa kahawa na ikasemekana mkulima atakuwa anahusika na kuuza mazao yake. Maoni yangu hapa ni kwamba hakuna mtu ambaye si mkulima wa kahawa atakayeruhusiwa kuhusika kwa njia yeyote na uuzaji wa kahawa. Ikiwa kuna mtu tayari amepewa leseni kama muuzaji wa kahawa na si mkulima wa kahawa, iondolewe. Corporate societies zipewe uwezo wa kuuza kahawa yao na iwe ni mali yao bila kuingiliwa na Serikali.

Kwa upande wa provincial administration, maoni yangu ni kwamba watu wote kuanzia P.C mpaka Sub-chief wasihusike

popote katika mambo ya kuendesha cooperative movement. Hiyo iwe kazi ya wale wamechaguliwa na wakulima.

Upande wa Health, yaani hospitali. Health services kwa wananchi wa Kenya ziwe basic human rights na Serikali igharamie. Kwa upande wa masomo ya secondary na post secondary education, fees ni kubwa sana mpaka katika chuo kikuu watoto wengi wanashindwa kuendelea. Tukiaangalia science and technology wanashindwa kuendelea kwa sababu watu ni maskini. Juzi kumbuniwa pararell programme, yaani private paying students, na fees ni ya juu sana. Upande wa masomo kuanzia nursery mpaka chuo kikuu, Serikali yetu ile itaundwa chini ya Katiba mpya ihakikishe kila mtoto awe wa maskini au wa tajiri, apewe nafasi ya kuendelea na masomo mpaka university, akiwa na uwezo wa kiakili. Kusiwe na upingamizi kama kwamba hawezi kulipa. Kwa mfano sasa wengine wao hawawezi kulipa shilling mia tatu elfu kwa mwaka wakasomee udaktari au elfu miatano kwa mwaka wakasomee udaktari. Hiyo iondolewe na iangaliwe kulingana na akili ya mtoto.

Kwa upande wa Katiba. Katiba yetu wakati huu inampa rais uwezo mwingi sana. Hiyo iondolewe. Uwezo wa Rais uweze kupunguzwa na Parliament. Yaani kile nasema hapa nikiongeza kwa kizungu Parliament iwe ina powers ya kuimpeach President akiwa amefanya makosa wakati anafanya kazi yake. Yaani precisely, ni kwamba Rais wa Kenya katika miaka ya kesho asiweze kukwepa sheria. Awe chini ya Katiba, kwa hivyo chini ya bunge. Hayo ni upande wa Katiba.

Katika upande wa kuandikisha wapiga kura, haya yanaletwa wakati wakati tunakaribia uchaguzi na hatuna wakati wa kutosha. Haya yaendeleo all the time. Wakati wowote waandikishwe wa wapiga kura. Voter registration. Electoral commission ipewe nafasi na uwezo zaidi. Ikiwa mtu amefanya makosa katika uchaguzi au pengine amelea fujo wakati wa uchaguzi, kundi hilo lipewe uwezo wa kumshika na kumshtaki kwa makosa hayo. Electoral Commission isiwe chini ya ofisi ya rais. Hili litupiliwe mbali na iwe na uwezo wake kikatiba. Pia ipatiwe pesa yake ya kuendesha shughuli zake kutoka kwa consolidated funds.

Jambo lingine nyingine nataka kuongezea linahusu barabara. Barabara zetu zinaharibika. Kile ningetaka kusema ni kwamba transportation, yaani usafirishaji wa mazao yetu hauwezei kaendelea katika hali hii. Ile kodi tunakusanya tunataka tuone inatufanyia kazi, inatufurahisha. Kwa sababu tunalipa kodi, barabara hatuoni, tunalipa kodi hospitali hazina madawa. Mambo hayo yarekebishwe kwa sababu ile pesa tunalipa tunataka tuone inatufanyia kazi gani. Hayo ndiyo maoni yangu bwana mwenye kiti. Asante sana.

Prof. Salim: Asante sana bwana Kuria, ungojea hapo kidogo, ah Commissioner Adagala ataka umwekee wazi mambo fulani.

Com. Adagala: Ah kwa education umesema PTA iwe recognized na sponsor?

Kuria: Sponsor; sielewi role ya sponsor maanake kule tumekuwa na mvurugano wa shule, sponsor hata haonekani. Kwa hivyo siwezi nikaongea mambo ya sponsor maanake yeye sponsor kwa hakika anaelekezwa na board. Ikisema watoto waende

walete pesa, yeye anakubali. Sijui kama ungetaka nikupe mfano? Niko na mfano mmoja ningekupa kama unataka.

Com. Adagala: Kwako---eh unajua shule zilikuwa za sponsors, hasa makanisa. Catholic church imesema inataka irudishiwe shule zake, na wengine pia. So may be, pengine mtu mwingine anayeelewa mambo ya sponsor angezungumza.

Interjection: ha

Com. Adagala: yeah, ni sawa tu.

Kuria: Hapo ningetaka kuongezea kitu kidogo. Mambo ya kurudishiwa shule hapo inakuwa ngumu kwa sababu community siku hizi ndizo zinajenga. Hata kama shule ilikuwa zamani ya kanisa fulani, na community ni watu ambao wako pale, si kanisa moja, kuna PCEA, kuna Anglican na wengine wamehusika katika kujenga shule, chuo. Wamejenga na watoto wao wanaenda huko. Tukirudia mambo ya kusema kanisa fulani ndilo lilikuwa lenye hiyo shule, tutaanza mvurugano sasa. Maanake zamani mimi nikumbukavyo nilipoenda shule, kulikuwa hivi. Ikiwa nyinyi mnashiriki na wazazi wako PCEA hamwezi kwenda Catholic. Tukirudi huko tutaleta mambo yale yale ambayo yalikuwako zamani na yakaondolewa. Kwa hivyo naona shule ziwe ni property ya community--- ok siyo za makanisa.

Com. Adagala: yes endelea

Kuria: Ah na---

Com. Adagala: No no sawa, hiyo imetosha. Lakini pia unajua haya tunayosema tumekisikia mahali pengi eh basic human rights, health education. Sometimes helping lakini ni wananchi ndiyo wanatoa kodi ili hivyo vitu viwe straight. Ijulikane kwa sababu watu wengi wanafikiri itatoka tu, lazima kodi itaenda juu. Hivyo ndivyo hutendeka. That is where the people are the government. So it is very important. Halafu unajua tumetembea hapa Kiambu na tumeona kila barabara ina lami na kuna mahali kwingine kama North Eastern Province, they have three kilometers of tarmac. Therefore they cannot, hawawezi develop kwao kwa sababu hakuna njia. Na pia provinces zingine zina pengine barabara moja inapita kwa province. Sasa eh pengine tujue tukizungumza pia tufanye balance kidogo. Sitageuza maoni yako lakini tujue pia Kenya is the whole of Kenya.

Kuria: Sijui kama ningengeza ya kwamba kile kitu nimeguzia sana ni kwamba hatutosheki. Hata kama kwingine hakuna, mimi maoni yangu ni kwamba ile Serikali tuko nayo hapa haikufanya ya kutosha. Kama ingekuwa imefanya ya kutosha huko kuna barabara moja katika province, pengine zingekuwa tano.

Prof. Salim: Asante sana Bwana Kuria Kagori kwa maoni yako, tafadhali ikiwa unataka maoni hayo yawe ya hiyo kuandikwa na ungependa yasomwe zaidi, tunaweza kuchukuwa hiyo lakini ulivyoandika hapa ni kwamba ni oral.

Kuria: Ah ni oral hii ilikuwa ni rough one.

Prof. Salim: Asante, asante. Thank you very much. Tukiendelea, basi kabla ya kuendelea mbele, kuna jambo moja inabidi nieleze. Ikiwa yuko kati yetu hapa ambaye ana taabu ya kusikia; semi-deaf or deaf, tunaye pia Lucy pale mwisho amekaa kwenye mlango, yeye ana kazi hii maalum, ana uhodari wa kuweza kumweleza ndugu yetu au dada yetu ambaye ana taabu ya kusikiza akamuonesha mambo yote, akamjulisha mambo yote ambayo yanasemwa hapa. Yuko mtu ambayo anahitajia msaada huo? Maana ni wajibu wetu iko kwenye sheria yetu kwamba lazima kila mwananchi aweze kufuata na kutoa maoni yake. Kwa hivyo yuko tayari na mukiwa mwamjua yeyote hapa ana taabu hiyo ya kutoweza kusikia au hasikii vizuri pia, tunaweza kumsaidia. Sawa. Tukiendelea mbele basi yuko bwana Samuel Kiburi wa PCEA Kiragina. Yeye ana memorandum na kabla kutupa, utapaa dakika tano tafadhali main points in five minutes. Kisha tutachukuwa memorandum yako. Point by point please. Kama alivyofanya mwenzako Kuria.

Samuel Kiburi: Thank you very much for being given this opportunity. My name is Samuel Kiburi Njoroge, and I am going to give a summary of few people in this parish who sat down and wish that these views be made known to you.

The first one is on distribution of land. In Kenya we have so many landless people who live as squatters while others have hundred of acres of land. The government has a lot of unutilized land. Therefore we find that every Kenyan should own between three to a hundred acres of land, including the landless or the squatters, people like chokora strolling in the town etc etc. We also looked at the land policy and said that the selling of land should be restricted by the government, to avoid making more squatters. This can be done by making sure that any landless person who has been allocated land by the government can only surrender it back to the government but cannot sell it.

Number two of the same is that: Kenya has a lot of semi-arid land that can be converted into valuable through irrigation. Therefore, this land should be irrigated to facilitate agricultural productivity. This should be done by the government to enable those allocated those pieces of land in those semi arid areas to go about their businesses of agriculture.

Number three is every land should be made accessible through road network, railway etc. We also said that land and other property ownership should belong to a man and his wife. That is, if one of them dies, the other one can take over the ownership, not just anyone. The wife above should be a legally married wife. B, Any Kenyan should have right to own any property including land anywhere in the republic of Kenya. C, grabbed government land should be re-claimed by to the government.

Then we have marketing of farm produce. Cooperative societies under the ministry of cooperatives development, should be empowered by the government to remain the only marketing channel of their farm produce. The ministry of trade should restrict imports to safeguard local industries.

Number four concerns executive powers. The Judiciary should be independent and should never be controlled by the President. The, vice President should be appointed by the President, sorry the vice President should not be appointed by the President but he should be elected by the Parliament. The Attorney General should be appointed by the Law Society of Kenya and then approved by the Parliament. The Commissioners of enquiry should be appointed by the Parliament and report their findings back to the Parliament, then to the public.

Five, the President should be:

1. Between 45-65 years of age,
2. Should be married or a family man,
3. Should have a recognized university degree
4. The President in power should not exceed two terms of five years each

There should be a Parliamentary calendar for government events, which should include election date, Parliamentary session, recess date etc.

Number six, constituents or members from a constituency should be given power to terminate the office of their MP. If found incompetent or if they are not delivering according to the constituents' expectations.

Number seven, our Kenya currency should bear the portrait of only one Kenyan leader instead of changing the portrait with a newly elected President.

Schemes of service that is number five, schemes of service for government organizations should be controlled to avoid favourism in some organizations.

The next number concerns natural resources. Conservation of land and of all natural resources should be enforced. Number seven, education system: there should be free primary education, to avoid primary school dropout due to poverty.

The last one, the type of government we advocated for or we recommend is a coalition government. That is all I had, on behalf of those few people in this parish, presided over by our parish minister. We had those views to present to you. Thank you very much for listening.

Prof. Salim: Thank you very much bwana Samuel Kiburi for your views, you can now hand over your memorandum to Mr. George Naholi but before you do that please Com. Adagala needs a point or two to be clarified.

Com. Adagala: Just as--- what did you say on portrait?

Samuel Kiburi: Ah I said that the portrait of our Kenya currency that is money, we said that it should bear only one President's portrait instead of changing every now and then. Because, formerly we had President Kenyatta our former President, now we have President Moi, we don't know who is going to take over next time. So may be someone else takes over and we will think about another portrait. We are going to incur a lot of expenses and it will also loose meaning thus history is going to loose meaning, as the history is going to be interfered with, as formulated by the founding father of the nation.

Com. Adagala: You know you--- money is always printed as they get old. From that what I remember there was a gradual change over; okay? So money will always be printed because it wears out.

Samuel: Okay

Com. Adagala: Yea. Ah then two, ah mh---

Interjection: Sorry, but even if money will be printed we would have wished that the picture of the President who is on the currency, we said that it should bear one President throughout, in history.

Com. Adagala: so why

Samuel: instead of changing the portrait, that is the picture---

Com. Adagala : But why would that be?

Samuel: eh

Com. Adagala: Why?

Samuel: ah we find that there is no need changing the---

Com. Adagala: it would have to be like the picture of the queen but even the queen, it changed from King George the sixth to the queen. You know eh I am not changing your idea but just you have to have a reason. It cannot just be ---

Samuel: doesn't change incur---

Com. Adagala: It would have to be a monarch or something.

Samuel: We think that we incur unnecessary expenses for changing the portrait and also for the history's sake.

Com. Adagala: From history we would have to show other Presidents. We are trying to talk about a hundred years. Like in the US the portrait of the President appears after 50 years of death. Like Kennedy has not appeared because it is not yet 50 years since he died. Yea, Clinton doesn't appear he is still alive, that kind of thing. So you would have to put a time like for instance if we say like 50 for the US, then even the founding father will not appear. Yea. So you need to have a little bit more reason than the practical reason of incurring expense because image is a very important thing and it doesn't matter how much it costs.

Dr. Mosonik: Thank you Commissioner, yea, I wanted to ask you about the vice President being did you say elected by

Parliament?

Samuel: Yea. I would think that he should be elected by the Parliament.

Dr. Mosonik: So that the President has no say over the election of somebody that he has to work with?

Samuel: So that he can be able to, also to serve those who have, ---ah – elected.

Dr. Mosonik: Okay. So I wanted to ask, you know Parliament will have many political parties and there will be one dominant political party may be which has got the most the members of Parliament. Is it is another way of saying the winning, the party with the most MPs will elect the vice President or what proportional of the votes do you have in your mind?

Samuel: You know, it is more or less like that, because the party that is going to have many representatives in the Parliament may be will automatically, with the number of votes come up with the vice President.

Com. Adagala: Okay, usually, bunge all over the world when they vote, they vote for a prime minister who is then in charge of government business. Yea. So this VP what could he be in charge, what could be his role? Because we are using the system for of electing a prime minister, for vice President. I am not changing it but I want to know what would his role be? Because he is a VP he is not a prime minister, what would his role be?

Samuel: Well I think since he serves under the President, and the President would have been appointed by the majority, I also think that there will also have been appointed by the majority. This will remove the evasion of some truth which we see in our country or may terminating his tenure him anyhowly. The President may terminate his services any time but if he is appointed--

Com. Adagala: I want to know his role. I understand the situation we have. I want to know what his duties would be. Because this is someone who has been elected by bunge and it is fine and of course it would be an election and it would be democratic and it is okay. What would his role be?

Samuel: I thought that his role would be exactly as that one of any other vice President.

Com. Adagala: Okay, it is okay it is your views.

Prof. Salim: Thank you very much. We move on now to first lady to give us her views this morning. She is Margaret Wanjiru. We would like as many ladies as possible to give views. We are enjoying, of course --- we are bound by our duties to make sure that a cross section of Kenyans give their views not only men but also women. Not only healthy men and women but also children and old people and disabled and minorities of all kinds. So twamkaribisha Margaret Wanjiru, is she here? Welcome Margaret. You are giving us oral views? In English or Kiswahili? In English. Karibu.

Margaret Wanjiru: My name is Margaret Wanjiru Mathu, and I would like to comment on the issue that has been going on in our country, concerning the women who have been married and after the death of their husbands they have been chased away, and their children. Because of that, the children suffer, even the women suffer. Because when they go back to their homes probably their brothers will not have space for them for inheritance. So I think it would be better for those women to be considered even though they have not conducted their marriages probably in the church or in the customary way. This is to avoid the suffering of the children.

Com. Adagala: Okay Margaret, in this country we have customary marriage it is called African marriage, we have Mohammedan or Muslim, we have Christian and we have statutory hiyo ya kuregister kwa AG au D.O au kwa D.C. Lakini eh how do you want them to be considered? Because they are married; they have children. Ah it is a section of society, they are married, they have children, you are saying they are married they have children (yes). Okay, how do you want them to be considered?

Margaret: To be the inheritors of their husband's property.

Com. Adagala: yea. They would have to either do customary marriage or the one where you register with the AG or the Kadhi. I don't know, inheritance is something very legal. So if the Constitution sets it, then it would have ---it would have to be a legal marriage. One, why haven't they registered when the husband is alive? May be the husband didn't want them to inherit. So it is these men you have to talk to. We shall consider your view. Perhaps the children can inherit because that is in the Successin Act if am not mistaken. In the succession Act, all recognized children are inheritants. Children can inherit because it is by right of birth, but if a woman and a man don't register their marriage, it is very difficult. I am not trying to do anything but I am just saying what you are saying is already in the succession Act, that the children can inherit. Okay?

Margaret: Okay

Com. Adagala: yea. Probably follow it up with a lawyer even male or female and see what it is like and make another submission, a written one because it is an important point. But if I don't have rights by birth as a child, then I have to have a right by law and that law will have to be registered. You have followed the law. Okay?

Margaret: Okay

Com. Adagala: You want the children to inherit or you want the woman to inherit? The widow. Including children?

Margaret: Both,

Com. Adagala: Both of them? But what I am saying is if you are unmarried, if you have not gone through customary or the registered one or any of those, then you end up not within the law. If you have to be married, she said, by custom, they haven't gone through the customary because that would give them the inheritance, and they have not gone through the Christian one. That is what she said. And then they have not registered, isn't it? with the registrar of persons?

Margaret: Yea.

Com. Adagala: You don't have a marriage certificate?

Margaret: yes

Com. Mosonik: I think what we are asking you, who is a widow according to your definition? Somebody who has just produced children or who is married in some way or you are proposing that any woman who produces children is automatically considered to be married and should inherit or what is the point? Relax kidogo, tell us, you are saying they are not married either traditionally or according to Islamic law or in any way and should still inherit. Is that what you are saying?

Margaret: But probably they get married, even though it was not in those ways.

Dr. Mosonik: Which other way would you suggest? May be she has a good idea. How else can you marry unless you go those ways? May be you have an idea.

Prof. Salim: Margaret you have heard the two Commissioners commenting on what you said. Do you have any further explanation to give us so that we understand it better? Have we understood you enough?

Margaret: yes..... (inaudible)

Prof. Salim: Did Com. Adagala represent your views faithfully? Are you talking about someone who is living with somebody and having children, he dies and she is left with the children and with no right to inheritance. That particular lady was not married to the deceased? She was not?

Margaret: Yes

Prof. Salim: She was not?

Margaret: She was married but not either in the customary or --- yes.

Prof. Salim: So what type of marriage was that?

Background: Inaudible

Prof. Salim: Just living together? But was it recognized customarily? Or was it customarily living together or just--- yea okay. Anyway I think everything was explained----(tape stopped)

Prof. Salim:telling us that she was married to a man, he then left her, got married to another lady, and but she was abandoned. That still a different type of problem but it is still a problem. So this area I think is very important for all of us and we welcome any views. Margaret if you go back, now think about it, you want to write to us? We can still receive written views from you in addition to the views you gave us today, and anybody else on that issue. Hopefully kina mama mmesikia jambo hili la widows who were left behind, and they feel aggrieved that their inheritance rights, and that of the children are not being taken care of. It is a very important matter. Asante, thank you Margaret. So we have to move on. and listen now to bwana Paul kamau Njuguna, who is also going to give us oral views. Karibu Bwana Njuguna, please these are oral views maximum 10 minutes.

Paul Njuguna: Yangu ni machache sana,

Prof. Salim: Very good

Paul Njuguna: Lakini mimi nataka kusema habari ya hiki kitabu, manifesto ya Kanu ya mwaka wa 1992. Mimi ni mmoja wa wale waliopigania uhuru, yaani Mau Mau. Hayo mambo yameandikwa hapa kwa page 61, kuwa wale walipigania uhuru, baada ya miaka thelathini na moja watapatiwa haki yao, kufuatana na maagano ya uingeraza na Serikali ya Kenya. Na sasa miaka thelathini na moja imekwisha na hatuoni mabadiliko. Kwa hivyo wale watu walikuwa misituni, jela, na detention, ndiyo wanaandikiwa hiki kitabu. Mimi sina mengi yangu ni hayo tu, kwa maana mengi yatasemwa na watu. Tuna hoja kuhusu kahawa na mambo mengine.

Com. Adagala: Ilikuwa mwaka gani hiyo manifesto?

Paul Njuguna: 1992

Com. Adagala: 92? Okay. Hata lete leta---(inaudible)

Dr. Mosonik: Unasema kwa sababu hiyo Serikali ya Kanu itaanzisha baraza la wapigania uhuru. Wanachama wa baraza hilo watatoka kwa majeshi na pia wawakilishi wa wilaya wa wapigania uhuru. Baraza hilo litatayarisha orodha ya kitaifa ya majina ya wapigania uhuru, na litakuwa na wajibu wa kuchunga maslahi yao. Serikali ya kanu itaanzisha mishoni maalum ambayo itapewa wapigania uhuru wote, wataandikishwa na ambao walipigana vita vya ukombozi, na pia itapewa kizazi cha wale ambao walifariki.

Com. Adagala: Sasa hii ni manifesto ya party. Eh jambo hili liko kwa Katiba?

Paul Njuguna: Sasa sitaweza kujibu hiyo swali kwa maana nilikuwa nakuja tu kutafuta njia ya hayo maneno.

Paul Njuguna: Unajua sisi tunatafuta kwako wewe.

Paul Njuguna: Ndiyo

Com. Adagala: Wacha niseme kwa kila mtu. Hatuna maoni sisi. Wala pengine ile kamati ya Njonjo ilikuwa na maswali, lakini hapa si maswali ni maoni. Sasa utwaambie maoni yako ili tujue hili linafaa liwe kwa Katiba.

Paul Njuguna: Maoni yangu ni hayo.

Com. Adagala: Hii ni manifesto ya party, that one you can ask Kanu but kama Kanu chairman yuko hapa unaweza kumuuliza. Lakini hapa, tunataka maoni yako ili tuendele. Tunasikia freedom fighters wana association. Kwa nini hamjataka hilo? Okay, twaambie pendekezo lako.

Paul Njuguna: Pendekezo langu ni tuonyeshwe njia ambayo kwaya tutaweza kupata haya maneno yameandikwa kwenye hiki kitabu.

Com. Adagala: wewe?

Paul: Sisi

Com. Adagala: Mimi si kuwa freedom fighter, nilikuwa miaka na tano siku hizo, I was five to ten years old. Wewe una maoni ambayo unaweza kutupa ambayo tunaweza kupeleka na kusema huyu Mr Kamau alisema hili na hili lifanyike? Litekelezwe.

Paul: Maoni yangu kwa hicho kitabu ni kuwa, tunataka tusaidiwe, tuone mambo yaliyoandikwa hapo kuhusu wapiganiaji yametimizwa.

Dr. Com. Mosonik: Hivyo ni kusema, hayo mambo kama yalivyoandikwa kwa hii manifesto yaandikwe kwa Katiba. Ndiyo hivyo unasema?

Paul: Ndiyo

Com. Mosonik: Unataka Katiba I--- okay.

Prof. Salim: Asante sana bwana Njuguna na tumeandika maelezo yako. Tukiendelea mbele tunamwita bwana Peter Mburu. Peter Mburu.

Peter Mburu: Wambere, ndathomire, nimambe matige kwaria njarie. Uria ukundafutira athii haria, giikare haha nguhe uhoro. Njitagwo Peter Mburu Njuguna.

Translator: Naitwa Peter Mburu wa Njuguna.

Mburu: Na gwitu ni guku Kiambu.

Translator: Na kwetu ni hapa Kiambu, Division ya Githunguri, sub-Location ya Kiratina.

Mburu: Na kwenda uthikiririe uhoro uri ngukuhe,

Translator: Nataka usikize habari nitakayokupa, yaani, mapendekezo

Mburu: Mawoni makwa wa mbere, ni uhoro wa kahua. Kahua nindatunyirwo ni andu matarimaga, na ngwenda jokerio ucio ni muti umwe.

Translator: Maoni yangu ya kwanza ni kuhusu wakulima walinyang'anywa kahawa, na mtu ambaye halimi, nataka nijibiwe.

Mburu: Muti wa keri, ni kahua ngagirio ndiyenderie.

Interjection: ----- inaudible

Translator: Ni kahawa. Eh anasema kahawa akishavuna akipeleka huko hapati, wakishapeleka huko kwa viwanda KPCU, hawapati matunda yake. Okay.

Mburu: Undu uria ungi, ni uhoro wa githomo kia University,

Translator: Ukwenda kahua gekwo atia riu.

Mburu: Ngwenda kahua njokeri, nii ndi murimi, njokerio kahua ndiyenderie.

Translator: Ningetaka wakulima turudishiwe kahawa ili tujiiuzie sisi wenyewe.

Mburu: Uhoro wa keri, uhoro wa University, thirikari yaigire uhoro ucio thiini wa town, kana barabara-ini, ni kii kiagiririe makirwo kundu matekuonana na raia, niundu nimathukagia indo cia raia? Mathukumite?

Translator: Jambo la pili, habari ya university, chuo kikuu. Serikali iliweka vyoo vikuu mijini kama Nairobi na kwingineko. Kwa nini hawakuleta huku reserve ambapo hatuwezi kuona wale wanafunzi wakikusanyika na watu wengine na kuharibu mali ya wananchi.

Mburu: makirwo mutitu-ini kuria mutitu kuria matekuonana na andu.

Translator: Wajengewe ndani ya misitu. Huko ndani hakuna watu wengi. (laughter)

Mburu: Undu uria ungi ni uhoro wa andu aria tuthuraga kajura kana MP, mathii thiini wa parliament, matiri bata naithui, ni undu ucio ngoiga, matwihia, twitikirio kumarutaga unangorwo no rucio. Ona councilor.

Translator: Jambo la tatu, ni kuhusu wale tunawachagua kama MP ama councillors. Wakiingia bungeni hawana haja na wale waliowachagua. Mapendekezo yangu ni kuwa tupatiwe uwezo wa kuwatoa, hata kama ni kesho hata councillors wenyewe.

Mburu: Muti uria ungi wa kana, aa

Translator: Jambo la nne,

Mburu: Andu othe thi-ini wa Kenya, tuigananio, tondu ciana ciitagwo chokora ciikaraga Nairobi, thirikari ndiciragia uhoro wa

andu acio ni andu, na maciarirwo ni andu, niki kigiragia andu acio maciarite andu acio, tuonio nia? Thirikari ithi inyite andu aciari a ciana icokie kuria cioimire.

Translator: Watu wote katika nchi ya Kenya, wasiwazishwe. Maana chokora, wale wanakaa Nairobi, wale hatufikiri kama ni binadamu. Kwa nini hatuonyweshi wazazi wa wale watoto wanao randa randa? Serikali ishike wale watoto na wawarudishwe kwa wazazi wao.

Mburu: Muti wa gatano, ni uhuro wa mbeba, itige gucoka gwitwo mundu atige gucoka kuhurwo thiini wa thirikari itigage kuhurwo kiongo kia munene uria urathana. Thirikari ithii icirie uria iriandikaga.

Translator: Tano, ni habari ya pesa, kuwa isiwe inawekwa picha ya yule anayetawala. Serikali itafute njia nyingine iandike kitu kingine hapo.

Mburu: Muti wa gatandatu, ni ciana tugwo ri kuhana okorwo ndi muthure ndi parliament nake uria ungi ni muthure no kiana kimwe giakorwo kina andu aingi, aria kiana kiria kiagia na rais wakio gikahe andu aya angi iti a Minister gitige gutuika noo marehuririra magayagire kwao tondu nigwo guthiaga.

Translator: Sita, ni vyama vya siasa. Wakati wa uchaguzi Serikali ipatie hao watu wengine nafasi, iwateue washirikishwe kwa Serikali.

Mburu: nayo mishara, wa mugwanja, mishara, igie kiana gia gwiciragia uhoro wa muchara ti andu mathiage kwihe mbeba kuria parliament nao alimu guku no thina marona.

Translator: La saba ni mishahara: chama cha kutengeneza mishahara kiundwe, si watu wengine kujiongeza mishahara na waalimu hapa wanateta. Mburu anasema kuwe na chama kinachoangalia mishahara yao ili watu wasiwe wakijiongeza mishahara na huku kwingine waalimu wanateta. Kwa hivyo hata waalimu wawe na kundi lao.

Mburu: ona inyui mwihau.

Translator: Hata nyinyi Makamisheni, mulisomeshwa na mwalimu.

Mburu: mwathomithirio ni mwalimu ona raisi uria wikuo, na aria angi a Minister mathomithitio ni arimu. Na nimamaimite mishara. Mamanengere mishara ya alimu.

Translator: Hata rais na wengine hata mawaziri wamefunzwa na waalimu. Mumewanyima mishahara wao. Waongeze mishahara ya waalimu.

Mburu: undu uria ungi nigetha ndikie, riu ningurikia, thiini wa Kenya, mundu wothe etikirio aikare oroharia angienda ndige kuhorwo uria ndirahurwo na guku ruguru kana Mombasa, ndathii

Mombasa nduike muraiya wa Kenya. Andu aria matari athomu maheo gitio ona .

Translator: Jambo lingine, sasa anamalizia. Hapa Kenya mwananchi akubaliwe kukaa mahali popote ambapo atapenda, asisumbuliwe. Na wale wasiosoma wapatiwe heshima yao pia. Nimemaliza yangu.

Prof. Salim: Asante sana mzee Peter Mburu Wanjuguna, kwa maoni yako, tumesikia, sijui kama wenzangu wana la ku--kwa ufupi kabisa kukuuliza ili tuendelee.

Com. Adagala: Mzee sisi watatu ni waalimu na tumefundisha hata ministers na mishahara yetu ya ualimu wajua iko chini sana

Peter Mburu: Kwa nini?

Com. adagala: Tutachukua maoni yako vile umesema.

Mburu: Eh?

Prof. Salim: Huyu hapa alikuwa ni mwanafunzi wangu, mimi ni mwalimu wake. Yeye sasa atakuuliza, nafikiri, jambo.

Dr. Mosonik: Hapana, sina maswala ila kusema kwamba tufikirie na tufahamu kwamba waalimu wanaanza nursery mpaka chuo kikuu. Vile umesema ni kweli. Asante.

Peter Mburu: Kikuyu dialect

Translator: Anasema kama kuna swali aulize. Iko swala?

Prof. Salim: Asante sana mzee. Tumefurahi. Thank you mno. Sasa bwana Mburu mwingine, huyu ni Maxwell Mburu. Karibu.

Maxwell Mburu: My name is Maxwell Mburu and I think I am not wrong when I am giving these views regarding the prison department.

Interjection: inaudible

Maxwell: Pardon? Yea, I have written here in a piece of paper, I think I am going to read them just for five minutes. We have the prisons which were designed during the colonial rule and as Africans we should have our own design giving us a more healthy and clean place.

Interjection: ----- inaudible

Maxwell: yea, we have criminals they are the rulers. When we get into the prisons, we find that they are the ones in authority instead of the wardens who are supposed to look after other people. Instead of these criminals now oppressing the other petty offenders or these other people who have done nothing, or lets say they are suspects taken into prison. You find that they are being oppressed by the criminals and murders who are there.

Interjection: ----- inaudible

Maxwell: It is a kind of racket/malpractice. When they get in there, they are the rulers and they are not asked any question. In this case I mean hard core criminals should be kept separate from these other criminals. They should occupy separate cells.

Interjection: ----- inaudible

Maxwell: Pardon? A murderer should be kept with another murderer similarly, a rapist should be kept with a rapist. That is to say a person who has committed such a crime should live in a cell where all the people who have committed the same crime are living. We have private bodies which I would like them participate in the rehabilitation of prisoners. For example here, there are churches which should participate in reforming the prisoners. Also other private body or any other organized group in position to rehabilitate the prisoners. We find many people coming out of prison retaining criminal behaviour, being more dangerous people to live with in the community. We have food which served in prisons, which is very unhealthy. It should be made better. I suggest a better way of life whereby prisoners are fed because they have a right to live.

Interjection: You are talking about all basic rights?

Maxwell: pardon?

Speaker: All basic rights for prisoner?

Maxwell: yea, basic rights yea.

Speaker: quality basic right

Maxwell: yea quality and healthy conditions and the use of disinfectants. Sometimes you find they just pour water, they don't use soap, they don't eradicate germs.(inaudible). Remand should be done away with. It was designed for the purpose of breaking the people so that when they go back in court they are in a position to argue concerning what they have done. In any case you find somebody, confessing a crime he never did, just because of the conditions found in the cells and the remand. Court procedure should be conducted in a way that a suspect is to be convicted and after the follow-up of the case they are punished according to their offense. So remands should be removed. These prisons should be made oral any way it should be

free. Bill should be introduced. Eradicate behaviour like sodomy, the prisons should declare any person who is a criminal as not fit to live with other members of the public. I mean that anyone who has been found to be a criminal should not live or the prison department should be given a law that will enable this person to be kept away from of the other members of the public because he is dangerous. Otherwise we find people going there and coming out here, doing the same things. So such precautions should be taken.

My other point concerns people who are dying in prisons, currently. Life is taken as in significant. I mean life in prisons and in any other place where somebody is to undergo court procedure, should be taken seriously and significantly. Aged people should not be kept together with these other young ones. People of different ag-groups should stay separately in prison. People who are aged in their own cell, middle aged people in another cell, and young boys and girls in their own cell, too.

The other thing is starving the prisoners, we have the prisoners who are starved.

Prof. Salim: Mr Mburu, sorry to interrupt you. You tend to repeat yourself in different ways. You are only talking in terms of prisoners welfare, their basic rights to food and that is what you are saying. So that is already covered.

Maxwell: Okay if at all it has been covered, it is okay.

Prof. Salim: And your time is up. Five minutes for those with written memorandum. We need the details, you can be sure of that. So if you want to wind up, ----

Maxwell: Let me wind up with the department of immigration. Anyone who is crime free for ten years should be issued with all documents to travel outside the country. A certificate of good conduct should be issued to anyone who is crime free for ten years. Fingerprints taken during domestic violence should not be considered if they were no killings or any other kind of hurting. That is all. Thank you.

Com. Adagala: What did you say about domestic violence?

Maxwell: Domestic violence, there are people whose finger prints are taken in the domestic violence cases. These fingerprints are taken to CID offices such that should this person like to travel outside or would like to have a certificate of good conduct, you find this person is not being issued the required documents because he was involved in a crime. This is not really a crime, it is just you know these violences that are always there and it is normal.

Com. Adagala: Do you think domestic violence is not a crime?

Maxwell: Domestic violence in some cases is not a crime because a woman, for example, may prostitute herself. Only to come home and may be in the ensuing misunderstanding, you may find that she is taking you to court of law and when your fingerprints are taken there, it means you cannot be issued with travel documents. Is that what you mean?

Com. Adagala: Eh I am shocked.

Maxwell: So am I

Laughter

Prof. Salim: Okay, we move on, bwana Joseph Waweru, asante kwa maoni yako na tukiendelea mbele John Mukui Njoroge. Yours is also an oral presentation eh?

John Mukui: I am John Mukui Njoroge from Gathogo sub-Location, Wamothai Location, Kiambu district. I want to start with the Presidential powers. The President is above the law and I want the powers of the President to be trimmed. He must not be above the law. There must be distribution of powers, such that even the vice President must be elected by the people. On education, there must be a provision such as free education for all people from nursery school to the university level. On health services, there must be free medical services. We should scrape this cost sharing. On land, nobody should own land more than 100 acres while others have nothing. There must be a limit.

Interjection: ----- inaudible

John Mukui: Nobody should own land more than 100 acres while others are landless. Yes. There must not be squatters in Kenya while land is lying unutilized. On local authority, let there be one county council---

Interjection: Prof. Salim: You have a recommendation on squatterdom? what do you want done about it?

Mukui: oh I want, I want to address squatters. There are people who are landless.

Prof. Salim: We know the problem, what is your recommendation, how do we resolve or solve the problem of squatters?

Mukui: Mimi ningependekeza ile mashamba imekaa huku bila kulimwa, hawa watu wagawiwe. On local authorities, there must be one county council and one municipality in one particular district, scrape all other urban councils. On agriculture, let farmers manage their cash crop especially coffee, tea and milk. On freedom of worship, in Kenya there is freedom of worship and I want to abolish this devil worshipping in Kenya. On political parties, there should be three political parties, that should be funded by the government. That is all.

Prof. Salim: Please wait there for a point of clarification.

Dr. Mosonik: Ningependa kukuuliza, maswali mawili. Kwanza umesema hekari mia moja iwe the ceiling. Sasa kama mtu ana zaidi ya hiyo na ilikuwa ya babu yake tangu zamani yaani ya family, wanyang'anywe ama ifanywe nini ama hii hekari mia moja igawanywe?

Mukui: Iuziwe Serikali igawie watu.

Dr. Mosonik: Walazimishwe kuuza shamba ya family, ile ya grandfather ile ile ya zamani.

Mukui: Pengine walipata hiyo shamba kwa njia isiyo halali.

Speaker: Ile shamba ya babu, kama hapa Komothai na kama inapita hekari mia moja hamsini yaani itolewe?
----- (inaudible)

Mukui: Naonelea mtu asiwe na hekari zaidi ya mia moja na mwingine hana. Pengine hiyo shamba, aliipata kwa njia isiyo halali. Kwa hivyo naonelea Serikali iingilie na ipatie wale watu hawana.

Speaker: Okay, la ya pili, umesema nini kuhusu haki ya kuabudu? Kwa gazeti la nation jana waliandika kwamba hatuwezi kuamua jinsi watu wenyewe wangependa kuabudu. Sasa Serikali ifanye nini kulingana na hilo kikatiba?

3. Mashamba. Tuseme Serikali ikitaka shamba ya mtu kama mimi au wewe awe anapatiwa shamba lingine kulingana na vile shamba lake lilivyokuwa hapo awali na hiyo gharama iwe ni ya Serikali. Kwa mfano, hiyo hospitali iliyoko hapa, na police iliyoko hapa ilijengwa hapa mwaka wa 1978. Wale walipeana hiyo mashamba yaani plot wakati huo, wengine hawajapata mashamba mengine hata leo. Wakati huo nilikuwa chief, na mimi ndiyo niliwapeleka wengine Kerita na wengine hawajapata mashamba hata wa leo.

Prof. Salim: Compensation kwa mashamba yaliyochukuliwa?

Harrison: Wananjia mimi mwenyewe wakiniuliza niliwafanya namna gani? Na hivyo ni kumwachia mtu taabu, aliye madarakani.

4. Ni wakulima kama wa kahawa, ama mkulima yeyote aachiwe madaraka kwa kile kitu analima. Ikiwa ni kahawa, tuna pendekeza pesa iende kwa mkulima mara moja bila kupitia vichorochoroni.
5. Minister apunguziwe madaraka. Kwa sababu hata mamboyakipitishwa na bunge, minister hujiongezea mambo yake. Yaani anachelewesha mswada. Hatekelezi upesi.

Prof. Salim: Siku ya kufanya nini?

Harrison: Siku, yaani wakati mswada umepitishwa na bunge na ukawekwa sahihi na President sasa minister anaongeza siku zile zilizotajwa.

Prof. Salim: Yaani anachelewesha?

Harrison: Anachelewesha.

Prof. Salim: Okay.

Harrison: Lingine ni la masomo. Masomo yawe ya bure. Serikali itoe masomo ya bure kwa sababu watu wasio na uwezo wa kifedha, hawasomeshi watoto.

Prof. Salim: Ungependelea education iwe ya bure?

Harrison: Iwe ya bure

Prof. Salim: Mpaka wapi?

Harrison: Tuseme kutoka standard one kwenda mpaka darasa la nane, elimu iwe ya bure kabisa. Kutoka pale kwenda hadi form four, mtu anaweza kugharamia masomo kidogo, bali Serikali itoe usaidizi mwingi ndiyo watu wote wawe na elimu ya kutosha.

Lingine, na ndilo la mwisho, wakati huu Serikali yetu tangu tulipopata uhuru imekuwa ikiteua kwa mfano, kama waziri wa afya na matibabu hospitali anafanyiwa ambaye hajasomea uuguzi. Kwa hivyo angependekezwa awe amesomea udaktari ndiyo awe akijua mambo kuhusu madawa inatazamwa namna gani, au hospitali inaendeshwa namna gani. Kwa sababu wengine hata wanatolewa kwa jeshi na waanapelekwa kwa hospitali. Mwingine anatolewa katika police anapelekwa kwenye ministry isiyo yake. Hayo siyo mazuri. Hiyo si Serikali.

Prof. Salim: Asante bwana Harrison Mwaura umesema kuwa hiyo ni mwisho?

Harrison: Ndiyo

Prof. Salim: Okay, thank you very much, asante kwa maoni yako. Sijui kama wenzangu wana swala lolote, Com. Mosonik, Com. Kavesta Adagala? Asante. Bwana John Muigai yuko? Amesharudi? Hayuko. Bwana Mbaa Moses:

Mbaa Moses: Majina yangu ni Mbaa Moses kutoka Gathinguru katika tarafa hii ya Githunguri. Jambo la kwanza ambalo ningetaka kupendekeza katika Katiba mpya ambayo tunaiunda sasa ni kwamba, ile Katiba mpya iandikwe kwa lugha ya Kiswahili kama itakavyoandikwa kwa lugha ya kiingereza. Sababu yenyewe ni nini? Sababu ni kwamba si wengi ambao wanaelewa Katiba ya sasa, kwa sababu hata kama kuna nakala za lugha ya Kiswahili ni chache sana na hazipatikani. Kwa hivyo tunasema Katiba mpya iandikwe kwa lugha ya Kiswahili na iandikwe kwa lahaja ya Kiswahili ambayo imesanisishwa yaani lahaja ya kiunguja. Na pia Katiba mpya ambayo inaandikwa kwa lugha kiingereza isiandikwe kwa lugha ya kiingereza kile cha zamani, Latin American, ambacho hakiiieleweki. Tunataka iandikwe kwa lugha ya kiingereza cha kisasa, yaani modern English. Hata katika biblia, tunapata biblia imeandikwa katika new international versions ambazo zinaeleweka kwa urahisi, Katiba iwe hivyo.

Kiswahili pia kifundishwe na kitahiniwe katika viwango vyote vya elimu. kuanzia darasa la kwanza, ama shule za chekekechea mpaka vyuo vikuu. Wale wote ambao wanasomea nyanja mbali mbali ambazo zitahusu uma kwa mfano wanaosomea kilimo, udaktari, pia nao wafunzwe kwa Kiswahili, ili wakija kuhudimia wananchi waweze kuelewana na wananchi moja kwa moja.

Pia, tunasema nini kuhusu sheria? Sheria pia iandikwe kwa Kiswahili, ambacho kitaeleweka ili kila mmoja wetu aelewe sheria inayomtawala na inayomfunga ili tusiwe watu wakukanganywa na mawakili wakitumia lugha nzito ambayo hatuilewi. Tunataka sheria pia ziweze kueleweka moja kwa moja.

Kuhusu elimu. Napendekeza ya kwamba elimu iwe ya bure kuanzia darasa la kwanza hadi vyuo vikuu. Sababu ni gani? Serikali in uwezo wa kuchukua ushuru na kuongezea ikaweza kutenga kiwango cha pesa ambacho kinaweza kukimu mahitaji ya elimu humu nchini. Na kama sivyo hivyo, katika shule za upili, basi tulipe Serikali ilipe 70% na sisi tulipe 30%.

Kuhusu mambo haya ya PTA. PTA tunataka iwekwe katika Education Act ili iweze kutambuliwa. Maanake mpaka sasa haitambuliwi. PTA imetajwa tu pale, na mzazi sasa ndiyo anayelipa pesa nyingi, ndiye ambaye anamlipia mtoto wake, ndiye ambaye ameweza kustawisha ile shule, lakini hasemi chochote kuhusu uendelezaji wa ile shule. Kwa hivyo tunasema nini? PTA iwekwe pale na ipatiwe nguvu ifaayo. Jambo lingine ambao nitasema ni hawa sponsors. Sponsor awe defined roles zake ni zipi katika shule. Anafanya kazi gani sponsor huyu? Anasponsor nini huko? Ieleweke vizuri sana katika Katiba ili tusiwe na hizi tafashani ambazo tumekuwa nazo, hawa wakisema hivi na hawa wanakataa. Ieleweke kila mtu ajue kazi yake ni ipi. Mfumo wa elimu uweze kuwapatia wale wote ambao wameupitia kazi. Vipi? Kupitia kwa Serikali. Iwe na sera nzuri ya uekezaji. Tuweze kupata viwanda vingi ambavyo vitaweza kuwachukua hawa watu ambao wanatoka katika vyuo vikuu, waweze kupata kazi. Ili tusiwe tunafundisha watu, tunawapeleka kule university, wasome shahada nyingi na halafu baadaye wanahama na kuwenda kufanyia wengine kazi. Tuwapatie kazi hapa.

Jambo lingine ni kuhusu kilimo. Katika sehemu hii yetu tuko katika ile tunaita agro-based economy. Kwa hivyo wakati ambapo kilimo kimekuwa na mtafaruku, basi tutakuja kuangamia. Serikali ibuni sera ambayo itakuwa ni imara, na ambayo itatuwezesha sisi kama wakulima, kuhakikishiwa ya kwamba tutapata soko kwa mauzo yetu, tutaweza vile vile kwa kupunguziwa vile vitu ambavyo tutatumia katika ukulima. Kama ni mbolea kwa mfano upunguzwe ule ushuru, uwe wa chini kiasi ya kwamba mkulima yoyote anaweza kuupata. Tusiwe watu wa kunyanyasa mkulima. Kama ni wakati ambapo tunapata mavuno mengi kuwe na sera ambapo Serikali itaweza kuweka katika maghala yake, halafu ikatoa wakati ambapo kuna upungufu. Si kusema kwamba kupata njaa halafu baada ya wiki mbili tatu hivi kumetangazwa twataka msaada. Haya hatutaki tena. Twataka sera nzuri.

Prof. Salim: Bwana Mbaa Moses wakati wako umekwisha kwa hakika nafikiri uko karibu kumaliza, labda point ya mwisho?

Mbaa: Yea katika kumaliza malizia,

Prof. Salim: Kwa ufupi kabisa tafadhali

Mbaa: Kuhusu pia kilimo. kwamba Serikali pia itoe pesa katika utafiti na uendelezaji wa kilimo. Siku hizi tunaongea kuhusu genetic modification, hatujazipata hapa. Uchina wamepata, mchele wanaweza kukuza hapa kwa wingi na kutuletea hapa

Kenya. Na sisi tunaweza kukuza pia kwa hivyo nasema tuwe na sera nzuri ambayo itawezesha tufanye utafiti na tuweze kukuza na kuinua kilimo chetu. Asanteni.

Prof. Salim: Asante bwana Moses Mbaa. Any comment, questions for him? Bwana John Ng'ang'a Kangethe.

John Kangethe: Asante sana Commissioners kwa kunipatia muda huu ili nitoe pendekezo langu kuhusu kurekebisha kwa Katiba ya nchi yetu.

Interjection: (Prof. Salim): Tafadhali jina lako kwanza, umeshasema?

John Kangethe: John Kangethe.

Prof. Salim: Pole pole sana

John: Nishasema, John Kangethe Nga'ng'a. Hata kama nilitumia address ya Nairobi kwetu ni hapa tu Kigumo. Pendekezo langu ni kuhusu Education Act. Ningetaka elimu iwe ya bure kutoka standard one mpaka standard eight ili tuondoe illiteracy. Kwa sababu hasa wakati huu, watoto hawasomi kwa sababu ya kukosa pesa. Lngine ni BOG, Board of Governors in secondary schools. I feel that this one should be abolished completely because they don't have funds to govern with, we have only funds to manage, which are contributed by the parents. Kwa sababu you find that those who are in the BOGs are old people, they don't have children in that given school, and yet they are decision makers. We feel that it is not proper that they should continue to run in the schools. The PTA should be empowered, be given a chance to run the school because they are the ones who contribute money towards the same exercise. What we have in primary schools should be applied in secondary schools.

Lngine ningetaka kuguzia ni kuhusu education, ni chancellor wa university. Hili lahusu Rais. I feel he should not be the chancellor, somebody else should be appointed by the university council to head the university. This should be somebody who is an educationist who knows what is to be done and what is required.

Hilo lngine ni juu ya creation of districts, divisions, constituencies, e.t.c. That should be determined by the population in a particular area because what we have now is somehow is biased. You find that an area where there are very few people is given a division or a constituency, something which it does not really deserve. While in other areas where you find many people, the administrative units are not there.

Prof. Salim: So what is your proposal?

John: That the divisions or the constituencies should be created according to the population of a particular area.

Lngine ni kuhusu wabunge wetu. I feel that most of the times they are not in Parliament yet they increase their salaries. There

should be a Commission which will look into their salaries, not themselves, because they are the lawmakers, they just pass anything, and it goes through and it is implemented immediately. So a Commission should be formed to review, to look after their salaries just like what we have in other bodies.

La mwisho ni juu ya judiciary and legislature. That the chief justice should not be an appointee of the President, because whenever there is a case the judgment will be is biased. He will be dictated to, by the person who has appointed him.

Prof. Salim: Here the question arises, who should appoint?

John: The chief justice should be appointed by the Judicial Commission.

Prof. Salim: Tafadhali bwana Kangethe John Ng'ang'a point of clarification.

Com. Adagala: We are a country of varied geographical and environmental diversity. Why do you want us to use only one factor to decide on administrative or political units? Because it could be argued that people who are over populated don't deserve to have special places. Are you saying when we will get there and will presenting this and there will be some people from Turkana they will probably be saying just that. For instance Turkana is the largest district in the country so it takes a very long time to go from one end of it to the headquarters. So those people are inconvenienced in that way. It is still large anyway, so why do you think we should use only one factor, population?

John: Eh my point of thinking is that the purpose of creating these districts and divisions is to bring the administration closer to the people. You find a place like Turkana and North Eastern, the place is scarcely populated, that means there are not very many people to be governed, yet in an area like Kiambu, there is no comparison--

Com. Adagala: So those people should have administration brought closer to them, isn't it?

John: Yes according to the number of people of people who are there.

Com. Adagala: So we can consider them non- Kenyans then?

John: No they are Kenyans but then--

Com. Adagala: Then you have to consider their environment?

John: Yea, that one should also be considered but actually it should be according to the population.

Dr. Mosonik: You know I think we are asking questions so that we are clear. You have said to bring administration closer people, not closer to many people. There is this question of Turkana, which we said is equivalent to three provinces, just as

one district in terms of area

John: yes.

Dr. Mosonik. Bigger than Nyanza and Western and Central combined in terms of territory. Then you know that they are backward there, there are no roads, no transportation. The other day we went to East Pokot, Baringo East and they have 3 divisions and to get to where we were sitting as a Commission, two men walked 60 km. Saa moja jioni wakaanza safari, walifika saa kumi na moja asubuhi, but only one arrived so as to be able to attend, and the others they cannot get there at all because hakuna barabara. There are no vehicles. They see vehicles only once a week, something like that. So if you are bringing administration don't you think you should consider factors like that? We are not disputing the question of population at all but we have got to get a kind of compromise as Kenyans so that everybody feels that they have been considered, fairly.

John: Yes, but then I don't see the need of bringing a D.O in an area where he will look after 30 people or 50 whereas in other areas you have about 2 thousand people and the D.O is very far from them. So I feel that the population should be highly considered.

Prof. Salim: It seems bwana Kangethe you want to do exactly what my colleague fears might happen. In other words in those areas which are huge but population is small you are saying that there is no need for such services, government services at all?

John: No no I don't mean that.

Prof. Salim: Well We've been told for example that a place like Ijara has only 7,000 people, and therefore it is not like some other places where the population is in thousands, tens of thousands and the hint given to us, is as if Ijara's 7,000 people or eight thousand whatever it is, that they don't need a representative to speak for them in Parliament. Okay can I put it another way, what is your idea of a figure we should determine the formation of a constituency?

John: It would depend on the potential in a particular area.

Prof. Salim: Mh

John: Yes, the average--

Prof. Salim: Okay, those are your views and we respect them. Thank you

John: Okay

Prof. Salim: Ah now we want to go back to the subject of diversity. We have heard someone purporting to speak for the mentally challenged this morning, can we then give the chance to someone who has come in late but he belongs to a group that has been marginalized and a group that we have been ordered by our Act to look into their welfare? Luckily at least there is

one. He is a physically disabled mwananchi and since we haven't heard one disabled person speaking for himself and his fellow disabled, I would like him to call him to come and give his views. He is Mr. David Njenga.

David Njenga: Thank you chairman and the guests. My name is David Njenga. I came here in the morning. I found somebody talking about the disabled, how disabled people are given responsibilities or any other thing. I would like to say that even those disabled, they can be given powers and authority to do anything, they can be even Parliamentarians. They have never seen a disabled person being a Parliamentarian or a councilor, why? That does not mean they are not educated. They are educated as everybody else but they are not given this opportunity.

Interjection: (Prof. Salim): Bwana Njenga, give us proposals as to how disabled can participate in everyday life in society or whatever else you feel you want to tell us. But give us proposals and recommendations. Are you talking in terms of the disabled in Kenya not having positions or in the world or ---

David Njenga: No sir I am talking about ----- (inaudible) which I know. In Kenya but not in the world---

Prof. Salim: My colleagues tells me that you are not aware that there are a lot of disabled people in important positions here in Kenya. But never mind, we don't want to but this, this is your chance to tell us about the problems of disabled and how they can be helped.

David Njenga: My proposal for the disabled is that -----(?) but most of them are not given priority to do they be given chance to compete with other people whenever there is anything to do. My proposal is that I have seen that in cooperatives if anybody messes about with anything of the public conducted connected with cooperatives, I don't know whether there is a law which concerns that.

I would like the Commission to have a law concerning mtu amechaguliwa kama chairman atakayenyakua vitu ya watu na anawacha hiyo company halafu cooperative inafunga. Mnasema inafilisika. Hakuna, huyo anaenda anakuwa tajiri. I propose kuwe na sheria ya kumfuata mpaka kwake nyumbani.

Prof. Salim: Kwa hivyo jambo hilo halihusu walemavu unasema tu kwamba yeyote ambaye amekula pesa za wanachi afuatiwe?

David: Afuatiwe mpaka kwake

Prof. Salim: Haya endelea

David: Wale wengine ni wasimamizi wa parastatal za hapa Kenya. Hata wao wafuatwe. Tumeona nyingi, zilifilisika na hatujui, sisi wenyewe zimefilisikaje. Hiyo sheria iwekwe kali.

Lile lingine ni tujaribu tusiweke pesa juu ya sheria.

Prof. Salim: Pesa?

David: Pesa hapana juu ya sheria. Siku hizi tunaonekana, tunaweka pesa juu ya sheria.

Prof. Salim: Asante hilo ni swala muhimu sana twakushuru na ungengojea kidogo wenzangu wana maswala kidogo kukuuliza.

Dr. Mosonik: Yea, ningependa kuuliza kukuhusu, jambo la kwanza ulilotaja: give priority to the disabled. Tukisema kuhusu bunge ama council, unawezaje to give priority to them? Tuseme kuhusu bunge how do you do that?

David: Tunalotaka sasa ni kuwa wakati wa election, tuiseme ni yule mtu mwenye nguvu tu. Mtu yeyote akiapply awe considered. Asiconsidered ati ni mtu ako kiwango aina gani, yuko na utajiri au nini, iangaliwe njia yote. Hapo ndipo nilikuwa nasema maana sijaona mtu wa aina hiyo hata akiwa na elimu zake.

Prof. Salim: Asante sana bwana David Njenga, twakushukuru kwa maoni yako. Na sasa namwita bwana Njoroge Kinuthia. Njoroge Kinuthia yuko? Hayuko. S.K Kimani. Bwana Kimani you have a maximum of ten minutes eh? But you don't need to use all of it.

S. Kimani: Yes. My name is Stephen Kinyanjui Kimani and I come from this Location. I have two points I want to raise which I will request the future Constitution to consider. These are: you see all of you go to the city and you see how the askaris are behaving. You might be walking you as a Commissioner and you meet a disabled person is selling something and he is harassed.

Prof. Salim: Mr. Kimani sorry to interrupt but we are all aware of the situation. Okay just refer to it quickly.

S. Kimani: I come to the judiciary. As a Christian these askaris can arrest me because of interacting. If I am taken to a police station, I am being told--

Interjection: (Prof. Salim) Sorry bwana Kimani, is that the second point?

S. Kimani: No no I am continuing

Prof. Salim: You are giving examples of harassment on the streets and now harassment of those arrested? What about the proposal? What do you want done, we are aware of it?

S. Kimani: Is that eh Okay

Prof. Salim: We can put it together as police harassment to hawkers and those who are detained and then give us your recommendations.

S. Kimani: Judiciary doesn't take care, if I am not a hawker and I am arrested if I deny "I am not drunkard" or "I didn't bhang" and for sure I don't. I am put in a cell for 14 days, in remand, and there is nowhere I can complain about this. And if you try to write to higher authorities, it seems you can be followed. So I propose there must be a Commission where we can be reporting this, where they can discuss each case.

The second one is about our roads. We have good roads they were built 20 years ago. The engineer has been given a budget each year for maintenance. He doesn't come and in case you are found sealing a pothole he can arrest you and you are put in a police station. I would propose that a Commission should be set where we should be reporting or complaining about the district engineer not using the allocated money in the budget in the right way.

Prof. Salim: Bwana Kimani in this way you are going to take a long time. Just tell us what things to be done about bad managers, bad engineers and bad contractors regarding bad roads.

S. Kimani: For the money he has earned through corruption, he should either be jailed if found guilty as a deterrent for them to fear to do such things. Second point is about education, I mean the third. We have got special children who are very intelligent. In other countries, there are special children so they don't go to university. We should have a Commission set to select those children who are intelligent or special in other fields. So we can have inventions of things, like Japan. If a child is even in standard four, if he/she is special in electricity there are places where they are taken. So we should have a Commission to look into that.

Prof. Salim: So what do you want to do with these bright young people?

S. Kimani: Sorry

Prof. Salim: What do you want to be done, what do you want the Commission to do? Once they identify this young people what do you want them to do with them?

S. Kimani: The Commission should be set to recruit people to run other industries after they have studied. The special children because--

Prof. Salim: Okay, these are geniuses, very bright young. But having they finished their education?

Kimani: I --

Prof. Salim: After they have finished their education? You see there are two aspects on this I am sorry to interrupt. We need to get things very clear so that we can take them round. You want a Commission set up to identify very very bright young

people, to educate them specially or to use them after they have been educated in very key industries in accordance with their qualifications? What are you telling us? Are you telling us the first or the second? In other words you are not clear on what should be done with these young people. Are they already graduates or they are those who are very bright in secondary schools and therefore they should be identified, to be educated in a special way.

Kimani: Right from secondary they should be identified rather than taking everybody to university.

Prof. Salim: Having been identified what should be done with them?

Kimani: It is the Commission to select

Prof. Salim: Having already selected them, what should they do with them, I have selected these five very bright people I am a member of the Commission and these are colleagues in the Commission. I have selected them what should I do with them?

Kimani: They should be given money to do research on what they are good at. Another point is about the hospitals. Our ministry of health has relaxed because some drugs which are brought here are for testing. And actually they have caused so much danger to people because they don't know. So I propose because each person if he is given the chance to oversee the selection, they will allow so many things to come in. It should be formulated. If it is hospitals or teaching university medical schools to discuss before a drug comes. That will help many diseases, which are coming.

Four, agricultural chemicals, which we spray. We don't have knowledge what they come to do. So I propose or either our research institutions are not doing the right thing. The Commission should be checking chemicals coming for agriculture because we might spraying some chemicals like vegetables. You may see a tomato in town it is so attractive and has been sprayed with a chemical which can cause cancer. Vegetables which you find actually so greenish and over this we don't have a say at all.

Prof. Salim: Joseph Kibe Ng'ang'a.

Joseph Kibe: Eh asante sana kwa kunipatia nafasi hii hili niseme machache hata ingawa mengi yamesemwa ambayo nilikuwa nahitaji kuyasema hapa kwa Commission. Ya kwanza ilikuwa ni kuhusu uwezo wa President. President wetu ana nguvu zaidi ya kwamba ni above the law. Ati hata akiniua hawezi kuulizwa. Tuwe na sheria ambapo President hatakuwa na nguvu, akitaka kuniua, anaweza kuniua, akitaka kuniondoa anaweza kuniondoa. Hivyo nikaona yuko na nguvu zaidi na ilegezwe kidogo. Pointi ya pili ni upande wa Ministers. Ministers wanachaguliwa na President. Kwa hivyo wanafanya vile wanaambiwa na President kwa sababu wako na uoga, hawawezi kufanya kitu ambacho kiko right ikiwa President hakitaki. Kwa hivyo naona wamepewa nguvu zaidi wawe wamelegezewa kidogo. Afadhali hawa wawe wakichaguliwa na Parliament yenyewe.

Vile vile upande wa judiciary. Nianzie kwa Attorney General. AG mwenyewe anachaguliwa na President na akichaguliwa na President--

Interjection: Prof. Salim: Bwana Ng'ang'a sisi ni wakenya tunafahamu mambo yote haya kwamba AG anachaguliwa na President. Sasa unataka nini? AG aendelee kuchaguliwa na President au achaguliwa na mtu mwingine au na chama au na board au nini? Tafadhali una dakika kumi na mimi baada ya wewe kusema nitajaribu kupunguza zaidi, badala ya kumi kidogo iwe hili ni muhimu, hili wote hawa waliojiandikisha wapate nafasi. Kwa hivyo maelezo hayo ya nyuma utaacha. Dokezea na kisha utoe pendekezo lako.

Kibe: Ningependelea kuwe na Commission kutoka kwa wale wa Parliament ambao tumewachagua sisi wenyewe, wawe ndiyo watamchagua. Sasa nitaingia upande wa kilimo. Sisi wakulima wa kahawa tuna taabu sababu hatuna nguvu ya kuuza mazao yetu mahali tunataka. Tunataka Commission iwape wakulima wenyewe nguvu ya kuuza mali yao mahali wanataka, bora tu wawe wanalipa Serikali tax ambayo inatakiwa yote. Kutoka hapo, kuna watu ambao sijasikia wakiguziwa hapa, watoto wanao tangatanga, ambao wengine tunawaita chokora katika mji wa Nairobi. Hawa ndiyo wamekuwa wakora, ni wabaya sana. Hawa ningependelea sheria itungwe ambapo Serikali itachukuwa hawa watoto na kuwaelimisha hili wawe watu wa maana kesho wasiwe watu wakusumbua wananchi.

Sasa ni upande wa wale watu wameritaya. Kwa mfano mimi nikiritaya nikifariki bibi yangu anapewa mshahara wangu kwa miaka mitano peke yake. Sijui ni kwa nini na bibi ni wangu na umri wangu ni wake nikifa asipewe hiyo pesa yangu mpaka afe. Kwa hivyo tutengeneze sheria ambayo itasimamia huyu bibi apewe mpaka afe.

Prof. Salim: Asante sana bwana Kibe kwa maoni yako ni wazi kabisa, na nakushuru. Samahani ilinibidi nikusukume kidogo mbele ili umalize haraka hili wenzako wapate nafasi. Asante. Nafikiri ningefanya hivi, ningetaja majina ya wale walio bakia, wale walioko au is it too early now? To divide towards time. Tuendelee kidogo. Bwana Gitau Kingere. Gitau Kingere? Hayuko? Bwana Francis Ngugi Kimani? Karibu.

Francis Ngugi: My name is Francis Ngugi Kimani, I come from Kiratina Sub-Location, Komothai Location. Pendekezo langu la kwanza ni juu ya term of Parliament ipunguzwe iwe miaka mitatu instead of five years. Tena tuwe na cheo cha prime minister na awe anachaguliwa na majority party in the Parliament.

Ya tatu. Okay ya tatu ni hii kuhusu health service. Hospitali hizi zetu za Serikali ziwe zinatoa huduma ya bure. Masomo ya nne, ya primary school kutoka standard one mpaka standard eight iwe ya bure. Lngine ni nomination of MPs, councilors isifanywe na Serikali. Hiyo iwachiwe raia wawe wanawachagua hao. Hii nyingine ni nominations ama appointing of chiefs of general staff, Commissioner of police, Prisons' Commissioner, hiyo iwe inafanyiwa na bunge. Isiwachiwe President sababu ndiye anafanya hiyo. Sasa hilo ingine ni kuwa Constitution hii ya Kenya ile itatengenezwa iandikwe kwa lugha ya Kikuyu

Background: laughter

Francis Kimani: Na nikimalizia---

Com. Adagala: Okay, Katiba kwa Kikuyu ni nini?

Francis Kimani: Kwa lugha ya Kikuyu

Com. Adagala: Katiba ni nini?

Francis Kimani: eh?

Com. Adagala: Kwa lugha ya Kikuyu

Francis Kimani: Katiba inaitwa aje?

Francis Kimani: “watho wa Kenya” Kikuyu dialect. Katiba ile tunatengeneza. Law

Com. Adagala: Lakini hii si law, hii ni Katiba

Francis Kimani: Si ndiyo

Com. Adagala: Si law

Francis: eh

Com. Adagala: Eh

Francis Kimani: Lakini ndiyo tunasema iandikwe kwa Kikuyu ndiyo tunaweza kuelewa vile inasema.

Prof. Salim: Nafikiri umeshamaliza?

Francis Kimani: Nimebakisha moja

Prof. Salim: Moja imebakia?

Francis: Eh nabakisha moja

Prof. Salim: Haya endelea, endelea ya mwisho

Francis Kimani: Ile inabakia ni---

Prof. Salim: Tafadhhalini ndugu hapa anatoa maoni na hebu tusikize kwa makini.

Francis: Hii case ya succession ambayo ilitengewa mahakama, huko inaitwa family division, inaweka case sana kama kwa miaka kumi, miaka ishirini na pengine yule anafanyiwa case alikufa zamani. Tunataka hiyo wakati ipunguzwe. Iwe kama miaka miwili, ndiyo sasa hiyo kesi isiwe inakaa sana huko.

Dr. Mosonik: Eh ni kwa Kikuyu peke yake ama lugha zingine kama hiyo?

Francis: Mimi napendekeza iwe inaandikwa kwa lugha ya kiingereza, hiyo iwe lugha ya taifa, na lugha ya Kiswahili. Lakini kwa sasa tunaongea juu ya hapa Githunguri si ndiyo mulisema? Eh sisi tungetaka iongeze hata lugha ya Kikuyu. asante

Prof. Salim: Yaani unaweza kukubali kwamba kila ikitafsiriwa kwa lugha nyingi ni bora?

Francis: Eh

Prof. Salim: Right

Francis: Kama kabila wale wanataka itafsiriwe kwa lugha yao itatafsiriwa

Prof. Salim: Kisomali, Kimaasai

Francis: Eh sisi tunapendekeza Kikuyu

Prof. Salim: Sawa

Com. Adagala: Ah unaelewa, unaelewa kama wale wengine ambao walipendekeza hivyo elimu ikiwa ya bure, matibabu ya bure, kodi itaenda juu, kodi itatoka kwa wananchi. Kwa sababu ile ilikuwa ya mbele ya bure na elimu na afya, ilikuwa inatoka kwa international loans. Lakini sasa ikiweko kodi kutoka kwa wananchi itaenda juu. Hata hivyo wananchi wanalipa hiyo loan.

Francis: Kama hapa sisi tunakuza kahawa na tunatoa hiyo kodi inaenda kwa Serikali. Tena wale wanafanya kazi kwa Serikali wawe wameajiriwa.

Interjection: (Com. Adagala): Nimesema itazidi kwa sababu sasa haitoshi hiyo, sasa itazidi.

Francis: sawa sawa.

Prof. Salim: Asante sana

Francis: Okay

Prof. Salim: Bwana Francis Ngugi Kimani kwa maoni yako, ilikuwa ni oral peke yake sio kwa mdomo? Okay. Kamau Ngeche, yuko? Kamau Ngeche? Edwin Gitau. Edwin Gitau? Hayuko. Robert Ng'ang'a

Robert Ng'ang'a: Asante sana kwa kunipatia nafasi ya kuongea hapa.

Prof. Salim: Karibu

Robert: Mimi niko na mambo mawili ama matatu. La kwanza, sisi tunataka Serikali ambao tunaitarajia kutawala karibuni imalize rushwa. Kwa sababu kila office ya Serikali kuna rushwa, kila mahali iko rushwa. Tunataka Serikali ya kumaliza hiyo rushwa.

La pili, hapa nchini kwetu Kenya kuko na wezi unaenea sana. Tunataka Serikali ambayo tunatarajia inakaribia kuja imalize uwizi kabisa. Tunasikia hata kuna Serikali ingine ya ng'ambo kama huko uarabuni, hakuna wizi, huko ni kunyonga ama kupiga risasi hadharani. Hatutaki mchezo, hakuna Serikali inaweza kuendelea ikiwa na rushwa na ikiwa na wizi.

Lile lingine la tatu ni la elimu. Shule zinafunguliwa January, mwezi wa kwanza. Na watoto wakienda kwa shule wanaambiwa nendeni mlete vitabu na ile vitabu tulinunua viko nyumbani tukapatia watoto waende navyo. Wakaenda huko wakaambiwa vimebadilishwa. Sasa hiyo vitabu kubadilisha kwa mwaka, hiyo sheria iundwe ya kusimamia kwa sababu ni kunyanyasa wananchi.

Prof. Salim: Asante bwana Robert Ng'ang'a kwa maoni yako hayo na ni wazi wazi kabisa. Ningekuambia kitu kimoja kwamba kwa hivi sasa mtu anayetumia silaha kuiba anauwawa hata hapa pia, au anatolewa hukumu ya kunyongwa ingawa anawekwa mpaka rais atakaposema haya mpelekeni anyongwe sasa. Maanake anangojea ruhusa ile ya rais ili anyongwe. Lakini sheria ya Capital punishment au ile ya kumnyonga anayeiba kwa kutumia silaha ni hiyo, ni ya kumumaliza kabisa. Haitoshi hiyo.

Robert: Anatolewa kwa kutumia pesa, kwa sababu ya rushwa.

Com. Adagala: Ningependa kusema tu kama mwalimu pia. Kuna nchi zingine, kama kitabu cha bayolojia au cha hesabu kinatengenezwa kinakuwa hard cover na kinadumu miaka ishirini, kumi na tano, ishirini. Ikiwa umenunua nyumbani au kwa shule. Sasa kweli mzee umesema kitu ambacho mtu mwingine hajasema. Ni kubadilishwa badilishwa kwa nini? Bayolojia inakuwa tofauti au ni nini? Mwali wa mtu umekuwa tofauti au ni nini? Umesema kitu.

Robert: Haya sawa

Prof. Salim: Haya, nikiendelea mbele, bwana Peter Kamweru yuko? Peter Kamweru? Haya. Kamweru. Bwana Kamweru you have a memorandum?

Peter Kamweru: Yes I have it

Prof. Salim: So where is it? Now you probably need to refer to it to highlight the points, only highlight no reading please. Since it is yours I am sure you know what is in there. Main points eh?

Kamweru: Haya. Mimi nataka kusema masomo ya --

Prof. Salim: Samahani utataja jina lako hapo

Kamweru: Peter Kamweru, nimezaliwa hapa kwa hii tarafa ya Githunguri katika huu mtaa wa Komothai. Na sasa mimi nataka kutoa mapendekezo yangu., Sasa nataka kusema habari za masomo: iwe bure kuanzia primary hadi university level.

Ya pili, tuko na watu wamefanyia kazi kijiji hii sana, tunawaita elders. Hawa watu wanatakiwa kuwa on pension kuanzia

------(inaudible) miaka ishirini na tano kwenda juu.

La tatu, tuko na watu wengine wako hapa, hawa watu disabled. Disabled ni watu kama wale wengine na wanatakiwa kuangaliwa sana sana. Kitu kile akifanyiwa yule, na yule mwingine pia anafanyiwa. Hata kulikuwa na mpango mwingine ulikuwa umefanyiwa lakini hawa watu------(inaudible) hiyo mchango ilifanyiwa. Ilikuwa ni harambee ilikuwa ya disabled. Bado pia haikuhudimia hao watu. Kwa hivyo tunaiuliza Serikali ishike huo wajibu sana na iangalie hawa watu disabled. Wawe wanapewa pension kwa kila mwezi ndiyo wanaweza kuendelea na maisha. Kuna watu weingine tunaweza kuongea juu yao. Tuseme habari ya hospitali. Hospitali ni lazima huduma ziwe za free. Tunataka kwenye Katiba ya leo ama ya kesho ile tunatengeneza sasa ziwe za bure kwa sababu watu wengi wanashindwa na ugonjwa inakuja kwa ghafla. Huna pesa ya Nairobi hospital, Aga khan na wapi.

Habari ya provincial administration, mimi naweza kusema hiyo imalizwe kabisa na instead wale watu tuna wachagua.....(?) Wanajua ile dawa..... (inaudible) ni lazima wawe wakiangalia na kuhudumia hawa watu kuliko wengine kwa sababu------(inaudible) pesa zote zinaokotwa katika wilaya hii, sasa zinapelekwa wapi? Zinapelekwa pale custody ya DC . Sasa hii pesa hujui inapelekwa upande gani? Ni zinafikia Serikali ni gani ambazo hazifikii Serikali. Hiyo hatujui. Kwa hivyo tunaweza kusema ile reason tunatoa iwe inaangaliwa sana na itolewe kama ni auditor general awe anatoa ile------(custody ya D.C)

Kuna lingine naeza kusema tu, habari ya basic rights. Hiyo nimemaliza basic rights. Habari ya Commissioner-----(inaudible) nataka kuongea juu yao kidogo. Hawa watu wawe wanachaguliwa na -----(inaudible) na wananchi wa Kenya. kutoka sehemu zote katika mikoa zetu nane. Kila mkoa unaweza kutoa wawili ama watatu. Lakini -----(inaudible) wasitoke kwa district moja. Iwe zote zinakuwa -----(inaudible). Na hilo neno la uchaguzi likiingia maneno inaenda----- (inaudible)

Kuna hii nyingine Commission ya human rights. Tunaweza kuongeza nguvu zaidi. Wakati hawa watu kama niseme ni police ama ni hospitali ama ni kotini ama ni kila pahali inahusu huduma za wananchi, hawa watu ni lazima wawe wanaingilia hayo maneno. Kwa sababu hawa ndiyo wanazijua shida za hawa watu. Kama wanafinyiliwa wanajua wanafinyiliwa. Kama hawafinyiliwi, wanaweza kutoa tu marekebisho kwa Serikali na waseme tunaka hii na hii. Huyu mtu, ambaye kwa mfano tuseme, hii habari ya magistrate, ni sheria hiyo na police iko hapa. Hivi Vinashikana. Huyu anakuja anatoa yule anamleta pande hii ingine. Sasa tuseme tuko na gari mnasema unroad-worthy vehicle, sheria yenyewe haisemi hiyo gari inatakiwa kufanyiwa nini. Inatakiwa kuwa dismantled ama inatakiwa grounded ama inatakiwa kufanyiwa namna gani? Ama ndiyo tunasema ni lazima iwe inatafsiri habari ya sheria. Ni kitu gani kitatendeka kama gari imeharibiki kabisa, au windscreen tu, basi kuwe na faini ama jambo lingine.

Prof. Salim: Tafadhali, tafadhali, hakuna haja ya details tupe mapendekezo. Recommendation

Kamweru: Habari ya President, hawezi kuwa juu ya sheria. Ya pili, hawezi tu pia kuwa juu ya mkuu wa wanajeshi. Ya mwisho nataka kusema, ni lazima tuwe na a public media ili sisi wote wananchi wa Kenya, watakuwa wanaitumia kupeleka shida zao ama maoni yao, kwa sababu, ikiwa tunachagua tuseme kama ni member of Parliament, labda hawafikii hawa watu ni lazima hajui shida za watu sana na yeye ndiyo anatuwakilisha watu huko kwa bunge. Tunataka tuwe na public media ndiposa mimi nikiwa na shida naweza kuenda kutoa maoni yangu yakaangaliliwe na ya mwingine pia. Asante.

Prof. Salim: Asante bwana Peter Kamweru kwa maoni yako na sasa ni multe bwana Mbugua Muturi. Karibu.

Mbugua Muturi: Shukrani sana, kwa kunipa nafasi hii niseme maneno machache.

Com. Adagala: Sema jina lako, okay

Muturi: Jina langu ni Mbugua Muturi. Kwetu Kathuruni, Kiratina sub-Location. Nasema hivi, Katiba tunaotaka kuunda kwanza jue kuwa Kenya kuna watu kwa sababu Katiba hii tunayo sasa haijui. Pili Katiba hii tunayoiunda sasa ituweke sawa sisi wote. Tatu, Katiba tunayoiunda sasa iwe inalinda mali ya wananchi wote.

Com. Adagala: Okay asante sana mzee. Hiyo itasaidia kwa preamble ni nzuri sana. Asante. Geoffrey, Geoffrey ako hapa? Okay.

Geoffrey: Asante sana Commissioner, majina yangu ni Geoffrey Kiarie kutoka Tabiroine, Kiratina Location. Yangu si mengi yale watu wengi wamekwishaongea zaidi yale ambayo nilikuwa nimetarajia. Lakini moja ambalo niko nalo ni ya ukulima sababu mimi ni mkulima. Ukulima tunaona hautiliwi maanani sana, sababu unaona watu ambao wanakuza mahindi, mahindi hayo hupotea. Kama sisi watu wa kahawa, hatuna nafasi nzuri ya kuweza kuuza mazao yetu. Lazima yauzwe na watu wengine, na hata watu ambao wanakuza mimea mengine hata hawa hawapati nafasi nzuri ya kuweka kilimo sawa sawa. Tunaonelea kama wakuzaji wa kahawa hakuna soko ya kuuza sawa sawa. Wakuzaji chai hata hawa wako taabuni pia wakuzaji wa miwa hata hawa wako taabuni. Tunasikia kuna sukari inapotea bure na ingine inakuja kutoka nje. Na tena wakulima ambao ni wafugaji, maziwa ya yanapotea, kwa kukosa soko. Na kuna maziwa ambayo tunasikia ambayo yanatoka nje. Sasa wakulima hawana uwezo, kwa hivyo Serikali iunde Katiba au section ya agriculture sector iwe sawa sawa. Watu wasaidiwe ili nchi hii na isiwe na hali ya kukosa vitu kama mahindi, maziwa kupotea, na kahawa kukosa soko.

Com. Adagala: Asante, haya asante mzee Geoffrey. Kuna William Kiarie? Ungependa kuchanga?

William: Kwa jina naitwa William Kiarie Gitau, mimi natoka hapa Kiratina. Nataka kusema machache maana ile nilikuwa nayo yameshasemwa.

Com. Adagala: Asante

William: Eh moja, nataka haki ya mwananchi, kwa hayo ninamaanisha ile siku tulipatiwa demarcation hapa, watu wamepata taabu sana. Ya kwanza mashamba iligawiwa na haikugawiwa kwa haki. Mashamba ile tuligawiwa hapa, demarcation

Com. Adagala: Mwaka gani?

William: 1950

Com. Adagala: 1950?

William: 1958

Com. Adagala: 1958?

William: Ehe

Com. Adagala: Okay

William: Kile mimi nataka kusema hapo, watu wale walifanya kazi hiyo walisahau mwananchi maana hawakugawa sawa. Mimi nikiwa na shamba hapa na mwingine yuko hapa, yaani watu walifanyiwa vibaya sana kwa mzunguko pa njia. Hawakupewa pahali ya kupitia.

Com. Adagala: Ungependa aje?

William: Kwa hivyo mimi nakaa hapa na hii ni nambari yangu na huyu ni mtu mwenye shamba hii na mimi nazunguka hapa kwote karibu maili moja. Sasa mimi kitu nataka hapa ni hiyo irudiwe watu wapewe nafasi ya njia.

Com. Adagala: Ungependa hivyo? Okay nyingine?

William: Lingine lile nilikuwa nataka kusema sana ni habari ya rais.

Com. Adagala: wananchi kuna jambo ambalo linafaa tuzungumze kwanza?

Background: inaudible

Com. Adagala: watu ambao wanazungumza, nani angependa kusema kile mnazungumza? Nani angependa kusema ili tujue kwa sababu sas inaenda-- amesema uongo?

William: Mimi nasema uongo?

Com. Adagala: Mimi nauliza amesema uongo?

William: kama mimi nasema uongo waje waseme vile mimi nataka kusema.

William: (laugh) mimi nilikuwa nauliza hivyo, ni swali nilikuwa nataka kuuliza.

Com. Adagala: Endelea, la pili huwezi kuuliza Katiba swali, sisi ndiyo tunakuuliza maswali. Wewe useme pendekezo lako.

William: Hilo ni pendekezo langu nilikuwa nalo, sasa lingine limekwisha semwa sana ni rais. Yeye ana uwezo sana. Hii nataka apunguziwe huu uwezo wake.

Com. Adagala: Okay endelea. Umemaliza

William: ah hapana. Lingine ni la hawa wajumbe wetu. Wakichaguliwa waje kutuona sisi wananchi. Maana kama sisi tunawachagua wanakaa miaka tano---

Com. Adagala: Ungependaje?

William: Mimi ningetaka wawe wakitutembelea sisi wananchi.

Com. Adagala: Sasa tutawafanyaje ili waje kuwatembelea kama hampendi, hampendi.

William: Akiwa hatembelei wananchi au hahusiani na wananchi tumuondoe.

Com. Adagala: Okay hiyo ndiyo Katiba kabisa?

William: Sawa mimi nafikiri hiyo ndiyo nilikuwa naye.

Com. Adagala: Hiyo inaitwa power of recall. Wananchi wanarecall wana power ya kurecall hayo yanaweza kuwekwa kwa Katiba. Lakini kama hampendi hatuwezi kuweka kwa Katiba. Lakini power iko. Anything?

William: No

Com. Adagala: Haya asante mzee, maoni yako yamesajiliwa. Kihara Mbugua. Njenga Wambiru, Njenga Wambiru? Okay.

Njenga Wambiru: Jina langu ni Njenga Wambiru kutoka Kibicho subLocation.

Com. Adagala: Njenga Wambiru endelea.

Wambiru: Kwanza ningesema kuna mambo mengine. Sijasikia hapa watu wengine wakisema. Kwa hivyo ningeuiliza kama tumefanya kitu kulingana na Commission hii ya Katiba. This imported farm goods, kama zinaweza kuwekewa high taxes kwa

sababu hizi ndizo zimeangamiza backbone yetu, yaani farming.

Com. Adagala: Pendekezo?

Wambiru: Pendekezo ni kuweko high taxes.

Com. Adagala: nini iwekwe high taxes?

Wambiru: Imported farm goods.

Com. Adagala: Okay

Wambiru: Chakula, kwa sababu ndiyo imeweka hii economy, backbone yetu vibaya.

Elections dates should be marked from when the Parliament opens. Kwa sababu hii election date, President ndiyo ana announce na announce wakati yeye inamfaa--

Com. Adagala: Hiyo inaeleweka, calendar kwa ECK, nyingine?

Wambiru: Lingine ni Ballot boxes should be transparent.

Com. Adagala: Lingine?

Wambiru: The President hawezi kuwa above the law. Hiyo iwe scrapped. Iwe scrubbed kabisa kwa sababu yeye ni mtu kama mimi amezaliwa hapa, tunavuta hewa moja, yeye awe kama mimi.

Com. Adagala: Haya

Wambiru: Akikosa makosa, koti ni moja.

Com. Adagala: Hiyo ni demokrasia, not above the law ehe?

Wambiru: Eh lingine ni juu ya PC, kiti cha PC, hiyo inatakiwa ninasuggest hiyo iondolewe. Halafu hata hivyo vya chief, assistant chief, badala yake kuwekwe elders, wazee wa kijiji wadogo wadogo.

Com. Adagala: PC nani ata---

Wambiru: PC?

Com. Adagala: Mh

Wambiru: Kwa sababu, instead of PC, D.C yuko kwa sababu yeye -----(?).

Com. Adagala: Asante, tuendele. Kimani Muiruri, okay come. Msikae mbali sana wale watu hawajatoa maoni, njooni karibu, tutachukuwa muda. Jina lako kwa Microphone.

Muiruri: Ehe asante sana kwa kuniita hapa niongee kidogo na nina furaha sana kwa wageni hawa wanakuja kututembelea. Kwa hivyo maoni yangu ni kuwa Serikali ilioko sasa management hakuna. Majority hakuna. sababu ndiyo hii: Nairobi kuna kiwete, kuna chokora hawa wa Nairobi. Viwete hawa kutoka asubuhi wanawekwa hapo wanauguzwa kwa jua. Chokora wanapiga watu kwa mawe na kuwapiga kinyesi. Watu hawa nataka wakamatwe, kwani watu wako normal. Chokoraa wanakula madawa hii ya kulevya. Wapewe mashamba acre tano tano--

Laughter

Muiruri: Kiwete hawa waandikwe majina na Serikali wapate kwao wajengewe duka. Serikali inaweka stock watu wao watakuwa wasaidizi wako wakitoka hapo. Nikiendelea nitasema hapa tangu zamani, kuna watu hawana shamba hata plot, hata acre moja hawana. Watu hawa kwa maoni yangu wapewe acre tano tano huko juu ya forest. Wapewe acre tano.

Nikiendelea ni mambo ya kina mama. Tunasema tunaoa wamama nyumbani na tunaoa ni kweli. Lakini wamama kufika nyumbani tunawatesa vibaya sana. Kwa vile kama kwangu nyumbani bibi yangu ninamtesa vile mimi nataka. Sina heshima mimi kwa bibi yangu. Bibi yangu naye kwa bwana yake hana heshima. Nataka kutoa maoni kutoka leo mabwana wako hapa na wakina mama, mabwana wawapatie bibi zao heshima kubwa. Akiwa ni bibi awe D.C, awe P.C, awe na heshima kwa bwana yake ndiyo wajue kulea watoto hawa. Tena iko taabu sana, wasichana wanaolewa, kama kwangu nimezaa wasichana sita, nane wanachukuliwa kakishazaa watoto tano, sita nikarudishiwa hapo. Yule mwingine vile vile, watoto wanakwenda kuwa chokora Nairobi. Wanakwenda kusumbua Serikali. Nataka kwa maoni yangu sheria ichukuliwe kali sana, mwenye kuzaa hao watoto awekwe ndani. Miaka mia moja hapana hakuna huruma.

Laughter

Muiruri: Sababu ni nini? Nilimaliza kulea –

Com. Adagala: Sikilizeni mzee tafadhali

Muiruri: Tena nikiendelea kwa mambo haya yetu ya wakulima wa kahawa. Akiwa ni mtu amechaguliwa hapa, anapelekwa kwa society anakula pesa ya wakulima yote, akasema wale walikuwako mbeleni walitolewa, walikula, walifanywa nini hata mimi nitakula. Mkiona hapa tuna taabu, tunaletewa taabu namna hiyo. Ni mtu akikula pesa ya mkulima hata ndururu mwaka mia moja, shamba anayo inauzwa na Serikali, atoke kwa barabara kwa sababu anaua watoto wangu. Na sio wangu peke yangu ni wa hawa wote kwa jumla.

Com. Adagala: Haya mzee endelea:

Muiruri: Kwa hivyo ndiyo nataka wachukuliwe sheria kali kabisa. Tena nikiendelea kwa malandlord, wenye nyumba, na ndiyo wenye sitima, mwenye kukomboa hiyo nyumba pesa ile anapata ni kidogo. Hata ya chakula haitoshi. Hata nyinyi mshahara ni duni, mimi najua. Mishahara mnayopata ni duni. Yafaa kupata kama ni karani, clerical officer apate elfu nane na pesa ya nyumba. Kwa hivyo land lord waonee huruma wenye kukomboa nyumba, hakuna pesa, Serikali inaingilia hii hata ikiwa ni plot yangu mwenyewe. Nyumba ni yangu na nimejenga, lakini hawa wenye kukomboa ndiyo wananiajiri mimi wakitoka pesa itatoka wapi, nitatoa pesa wapi wakitoka wote? Hawa ndiyo watajiri wangu na mimi niwaonee huruma. Nikiendelea mambo ya elimu.

Com. Adagala: ya mwisho?

Muiruri: Eh ya mwisho.

Com. Adagala: endelea

Muiruri: Mambo ya elimu kutoka standard one mpaka university ni mambo ya Serikali. Wazazi waondokewe na karo kwa vile watoto wanafukuzwa kila mara. Watoto wangu sasa hawasomi, walifukuzwa wote wako nyumbani. Kwa hivyo kwa maoni yangu soko hii tunataka ijengwe, iwekwe ukuta, wajengewe wawekewe mabati kwenye kuuza nguo, nguo zao zisipate pata matope.

Com. Adagala: Nani ajenge?

Muiruri: County council. pesa wanaitisha ya nini? Bibi yangu anatoka na fees akiingia hapa anaambiwa leta pesa. County council ndiyo itajenga pesa wanachukua za nini?

Com. Adagala: Okay taxation okay

Muiruri: Tena, barabara hii, barabara hata ukipita hapa ni kama barabara ya ng'ombe. Na mwenye gari, kodi yake kubwa, kwa hivyo barabara iwekwe lami na itawekwa.

Com. Adagala: Okay

Muiruri: Daraja iko hapa hakuna daraja zilijengwa zikahesabiwa ni mamillion na ni daraja ya kupita baiskeli

Com. Adagala: Okay asante mzee, hata hiyo ya daraja tumechukuwa. Haya asante. Asante kwa kuchanga mzee na moyo wote. Francis Mburu Gachukia, Francis Mburu? Ernest Mukaru? Okay njoo haraka haraka. Sema jina lako kwa microphone.

Ernest Mukaru: Eh mimi naitwa Bwana Ernest Mukaru Kanage, nilizaliwa katika wilaya ya Kiambu, katika Githunguri division. Kwangu nyumbani ni Komothai Location ndipo ilipokatwa nikaingia katika Location ya Kiratina. Yangu ni machache.

Kuna kitu sijasikia kikitajwa na yeyote aliyeingia hapa tangu asubuhi. Tuna watoto wamezaliwa kila mwaka na upande wa kupata vote, kadi za uchaguzi, tumepewa mwezi mmoja. Hakuwezekani watoto wazaliwe mwezi mmoja. haiwezekani. Hizo card ziendelee kupeanwa hadi mwisho wa mwaka kwa sababu watoto wetu wakati kama huu tunaelekea kwa uchaguzi, wanang'ang'a nia kwa kitambulisho hakipatikani. Wanan'gang'ania kwa kupata vote hawawezi kupata pia kitambulisho. Hivyo mimi napendekeza, hayo mambo yachunguzwe na Commission muchukue hayo mambo kama ni kitu muhimu.

Nina mambo mawili tu. La pili, katika mkoa wa kati, sisemi hali ya Kenya Nzima. Ninasema katika mkoa wa kati.

Com. Adagala: Ngoja mzee haujatwambia tufanye nini na--tufanye continuous registration?

Ernest: Yea.

Com. Adagala: Haya endelea mukoa wa kati.

Ernest: Nimesema katika mukoa wakati, kuna watu wana Location kama sita katika shamba wanalo kama, acre elfu tano, sita. Kuna watu wengine hawana. Wanajaribu kurithi ya babake acre mbili wagawane watu ishirini. Watoto wao sasa ni wazima, wanataka nao niwakatie plot niliopatiwa na baba na haiwezekani kwa sababu sina nguvu ya kujenga gorofa. Hata ukisikia watu wakisema hapa kuna chokora kuna chokora, chochote upandacho ndicho uvunacho. Kwa hivyo ninapendekeza katika wilaya ya kati, mtu yeyote aliyezaliwa hapa kama citizen wa hapa, apewe acre, kila mmoja citizen wa Kenya.

Com. Adagala: Ngoja mzee hapa unasema mtu aliyezaliwa hapa Central province?

Ernest: Mtu alizaliwa hapa Central province

Com. Adagala: Apewe heka ishirini hapa central province?

Ernest: Akitoka Central province, atapewa vile watu wa kwenu walitenga. Akitoka hapa aende Rift valley atapewa vile watu wa Rift valley waliamua lakini sisi hapa ni ishirini.

Com. Adagala: Hiyo siyo, ninasema ambaye alizaliwa hapa apewe acre ishirini hapa

Ernest: Hapa. Akihamishwa kwa sababu shamba itakwisha akienda kule ama pande hii kwa kuchunga si kwa wakulima, aende kwa kuchunga, atapewa vile walivyopima wenye kule. Sasa sisi tukikata kauli, tutasema D.C, D.C ndiyo ni mzuri lakini hatumwingilii ataingiliwa na Katiba tu.

Com. Adagala: Asante mzee. Any? Haya enda huko mzee. Afuataye ni Edwin Gitau. Edwin Gitau? Kama hayuko Rebecca yuko? Okay Robert Ng'ang'a? alitoa na naona amemark hapa. Joseph Kigura, Joseph yuko? Haya hatua kwa

hatua njoo hapa utoe maoni.

